**ASKOFU** Mdegella aonya kushamiri kwa vitendo vya utekaji, mauaji
UKURASA 3



**WAGONJWA**, ndugu wamlilia waziri gharama kubwa matibabu MOI
UKURASA 3


**DK. MWINYI** ataja viashiria vya awali aina 11 za madini visiwani Zanzibar
UKURASA 17




UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Septemba 13, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581798
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# LATRA yatishia kusitisha usafiri wa mabasi usiku



UKURASA 2

UKURASA WA 23

## COASTAL UNION YAMKANA MGUNDA

KLABU ya Coastal Union imekana kutaka kumrudisha kocha wake wa zamani, Juma Mgunda ili kukinoa kikosi hicho. Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema taarifa za Mgunda kutaka kurejea...

## Vurugu madai ya uvamizi kituo cha polisi zaua watu wawili

UKURASA 2

## Mpango azindua jengo huduma upandikizaji mimba

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akisikiliza maelezo kuhusu namna ya upandikizaji mimba kutoka kwa Daktari Bingwa wa Upandikizaji Mimba, Dk. Chuor de Garang Alier baada ya kuzindua kituo cha upandikizaji cha Dk. Samia Suluhu Hassan katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

**MICHEZO** NDUMBARO AITAKA TAIFA KRIKETI KUFANYA VIZURI UK 20
MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Masuguru, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa na furaha baada ya kumaliza Mtihani wa Taifa, jana. Jumla ya Wanafunzi 5,576 walifanya mtihani huo wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# LATRA yatishia kusitisha usafiri mabasi usiku

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imetishia kusitisha safari za usiku kwa mabasi yanayokiuka masharti, kanuni na taratibu za usafirishaji.

Ukiukwaji wa kanuni hizo umeelezwa kuwa ni chanzo cha ajali, vifo na majeruhi kwa abiria.

Kadhalika, mamlaka hiyo imetoa siku saba kwa mabasi ya Super Feo, Abood na BM kujirekibisha kabla hayajasitishiwa leseni za kutoa huduma baada ya kubainika kukiuka masharti kutokana na kusababisha ajali mfululizo.

LATRA pia imesitisha utoaji huduma kwa mabasi yote ya Katarama kwa muda usiojulikana mpaka kazi ya kuyachunguza itakapokamilika.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, mabasi ya Katarama yanatuhumiwa kufanya hujuma ya kuchezea mifumo ya kufuatilia mienendo ya mabasi (VTS) na mifumo ya kutoa taarifa (I. Button) na kufunga vifaa vyake ambavyo havijulikani ni vya modeli gani na si vile ambavyo vimethibitishwa na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS).

Suluo alitoa uamuzi huo jana kwa waandishi wa habari baada ya kikao chake na baadhi ya wamiliki wa mabasi ya masafa marefu yenye uwekezaji mkubwa katika eneo hilo ambayo hivi karibuni yameonekana kufanya makosa na kupata ajali mfululizo kwa mabasi ya BM, Super Feo na Abood.

"Mtakumbuka kwamba tunakaribia kutimiza mwaka mmoja tangu tuanze safari za usiku. Serikali ilifanya uamuzi kupitia Mkutano wa 11 wa Bunge, Juni 28, mwaka jana kutoa ruhusa kwa mabasi kusafiri nyakati za usiku na ilitoa maelekezo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi kuweka utaratibu wa kutumia kwenye safari hizo za usiku.

"Tangu kipindi hicho mpaka Septemba mwishoni taratibu ziliaanza kuwekwa na sisi kama Wizara ya Uchukuzi tulianza kushirikiana na wadau wetu na hasa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), ili kuweka utaratibu na mojawapo tulizoweka ni kuwataka watoa huduma wasaini tamko la kukubali masharti ya leseni wanaposafiri usiku," alisema Suluo.

Alisema yako masharti saba ambayo wasafirishaji hao walikubali na kuyatia saini kwa ajili ya kupewa kibali cha kutoa huduma ya usafirishaji usiku na kwamba, ili kukidhi kupewa kibali hicho walitakiwa wayakubali na wayasaini lakini baadhi yao licha ya kufanya hivyo tayari wameanza kuyakiuka.

Alitaja masharti hayo kuwa ni pamoja na kutia saini tamko hilo la LATRA na kulikubali, kuunganisha mabasi kwenye VTS, madereva kupokezana kwenye safari za zaidi saa nane, madereva kusajiliwa na kuthibitishwa na kupewa kifaa utambuzi (I,botton).

Mengine ni kuwa na ofisa mahsusi ambaye jukumu lake ni kufuatilia mabasi ya kampuni yake, kutoa taarifa sahihi za abiria wanaosafiri, mizigo kuwekwa alama ya utambulisho ya mhusika, kutoruhusu asiye abiria kupanda kwenye gari kabla na wakati wa safari.

"Kwa hiyo baadhi wameanza kukiuka masharti hayo na sisi kama LATRA kwa mamlaka tuliyopewa na sheria, tunatakiwa kuwalinda Watanzania, hatuwezi kuvumilia kuona masharti haya yanakiukwa.

"Hizi ajali zinavyotokea ndugu zangu, vifo, majeruhi havikubaliki, mtu mmoja tu akifa kwenye ajali hata muuze mabasi yote ya nchi hii kurudisha roho ya yule aliyefariki kutokana na ajali haiwezekani, kwa hiyo tusifurahie au kuona ajali imetokea halafu eti mnasema amefariki mtu mmoja tu, hiyo roho ya mtu mmoja ina thamani kuliko mabasi hayo yote, mtu asikie uchungu ndani yake kwamba ninapoteza uhai wa mtu kwa biashara yangu," alisema.

DAR ES SALAAM GYMKHANA CLUB

**NOTICE OF THE HALF YEARLY GENERAL MEETING 2024**

**[Issued under Article 13 of the Dar es Salaam Gymkhana Club Constitution, 2017]**

NOTICE is hereby given that the Half **Yearly General Meeting** of the Dar es Salaam Gymkhana Club will be held at the roof terrace of the Club on **Thursday 19th September 2024** commencing at **6:00PM.**

**AGENDA:**

1. To read the Notice Convening the Meeting and confirmation of the agenda.
2. To confirm the Minutes of The Adjourned Annual General Meeting held on Thursday 25th April, 2024
3. Matters arising from 2 above.
4. To receive the Report of the Management Committee in accordance with the Article 13(b) (ii).
5. At the discretion of the Chairman, to consider any other business of which the Half Yearly General Meeting is competent to discus

**Issued in Dar es Salaam this 29th day of August, 2024**

**By Order of the Management Committee.**

**Honorary Secretary**

# Wauawa madai kuvamia kituo cha polisi Geita

**Na Vitus Audax**

JESHI la Polisi limesema limewaua watu wawili kwa risasi wakati wa vurugu zilizotokea katika Kituo cha Polisi Lulembela, Mbogwe mkoani Geita.

Vurugu hizo zinadaiwa kufanywa na zaidi ya wananchi 800 waliovamia kituo hicho wakiwataka watu waliohisi kuwa wezi wa watoto.

Waliouawa katika vurugu hizo wametajwa kuwa ni pamoja na mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Lulembela, Teresia John (18), mkazi wa eneo jirani na kituo hicho cha polisi na mwanamume anayekadiriwa kuwa na miaka 18 hadi 20 ambaye majina yake hayajatambulika.

Taarifa iliyotolewa juzi na Msemaji wa Jeshi hilo Makao Makuu Dodoma, Naibu Kamishna (DCP) David Miseme, ilibainisha chanzo cha vurugu hizo ni watu wawili walioonekana wakiwa wamebeba watoto wawili katika eneo la mnada wa Lulembela na kuhofiwa na wananchi hao.

"Vurugu hizo zilianza katika mnada kisha kuhamia katika kituo cha polisi majira ya saa 8:39 mchana ambako wananchi hao baada ya kuona watu waliobeba watoto, waliwahisi kuwa wezi wa watoto na kuanza kuwashambulia," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, baada ya kuanza kuwashambulia, alitokea Mtendaji Kata ambaye aliwabeba kwenye pikipiki na kuwakimbiza katika kituo cha polisi.

"Baada ya watu hao kufika katika kituo cha polisi watu wanaokadiriwa kuwa 800 walifika kituoni hapo na kuwataka askari polisi wawakabidhi ili wawaue," iliongeza taarifa hiyo.

Baada ya hapo inadaiwa kuwa, polisi waliwazuia na kuwaelimisha juu ya makosa ya kujichukulia sheria mkononi lakini wananchi hao walianza kushambulia kituo cha polisi kwa mawe wakitaka watolewe.

"Mbali na kushambulia kituo na kutaka kuingia ndani, wananchi hao walichoma moto gari moja lenye usajili namba T.440 ATW aina ya Toyota Cardina lililokuwa limeegeshwa nje ya kituo hicho," ilibainisha taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema baada ya kuwapo kwa hali hiyo, askari walianza kutumia mabomu ya machozi na baadaye silaha za moto kwa kupiga risasi juu ili watu hao watawanyike hali iliyosababisha kuuawa kwa watu wawili waliokuwa katika eneo hilo.

Hata hivyo, ilibainika kuwa watu hao walikuwa wamebeba watoto wao na wala hakuna aliyekuwa ameiba mtoto. Taarifa ilibainisha kuwa Emanuel John (33) alikuwa amebeba mtoto wake Ikram Emanuel (mwaka mmoja na miezi 11) na Ng'amba Leonard (24) alikuwa amembeba John Emanuel mwenye umri wa miaka miwili na miezi minane.

Mama wa watoto hao, Rachel Masunga (22) alithibitisha kuwa watoto hao ni wake na walikuwa kwa wifi yake walipofuatwa na baba yao mzazi na mjomba wao.

DCP Misime katika taarifa hiyo alisema jeshi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo sambamba na kukamata wanaodaiwa kuhusika katika vurugu zilizosababisha vifo hivyo.

HABARI KITAIFA

# Mpango azindua jengo huduma upandikizaji mimba

**Na Christina Mwakangale**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema uzinduzi wa huduma ya upandikizaji mimba (IVF) ni msaada mkubwa kwa wananchi na familia zilizokumbana na changamoto ya uzazi kwa muda mrefu.

Alisema awali ilipatikana nje ya nchi kwa gharama kubwa na sasa huduma ya IVF nchini inatarajiwa kugharimu takribani Dola za Marekani 5,000 (sawa Sh. 13,611,700) kulingana na aina ya matibabu.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akizindua jengo la Upandikizaji Mimba (IVF), kupokea gari la kliniki tembezi (mobile clinic van) pamoja na kuwasha mashine za vifaa vya usikivu kwa watoto 14 (cochlear implant) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Ni wakati wa nchi kujitegemea katika tiba za kibobezi zinazotolewa na wataalamu wa ndani ili kuwapunguzia gharama kubwa za matibabu ya kibingwa Watanzania.

"Serikali itaendelea kujivunia na kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani namna ya kuvitumia vifaa vya matibabu ya kibingwa pamoja na kupatiwa ujuzi wa kuvikarabati pindi itakapohitajika," alisema Dk. Mpango. "Mradi huu ulianza mwaka 2019 na umegharimu Sh. bilioni 1.1 mapato ya ndani. Ni faraja kubwa huduma ya upandikizaji IVF kuanza kutolewa kwa mara ya kwanza nchini katika hospitali za umma, awali ilipatikana hospitali binafsi pekee, Arusha na Dar es Salaam, wengine wakienda Afrika Kusini, Uturuki au Kenya."

Kuhusu huduma ya upandikizaji vifaa vya usikivu, kabla ya mwaka 2017, alisema awali haikupatikana nchini na iliwalazimu wenye mahitaji kwenda nje ya nchi kwa matibabu, hatua ya kuanza kwa huduma hiyo ni kuwapunguzia gharama wananchi za kufuata matibabu ya kibobezi nje ya nchi.

"Nawaomba wataalamu wetu wazingatie watoto hawa kujifunza kuzungumza 'speech therapy' ili watoto waliopandikizwa 'cochlear implant' waanze kuzungumza," alisema Dk. Mpango.

Alisema hatua ya MNH kuwa na gari la kliniki tembezi, itaboresha huduma na kuwafikia wagonjwa walipo, pamoja na kukamilisha azma ya hospitali za matibabu ya kibingwa kufanya huduma za aina hiyo mara nne kwa mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema mradi wa IVF utaanza kwa kuwapandikiza mimba kinamama 10 ambao wamekwishaanza kliniki, kuna wataalamu 10 na uwezo wa kituo hicho ni kutunza mayai kwa zaidi ya miaka 30.

"Kama lilivyo jina letu la Hospitali ya Taifa tuliona familia kushindwa kupata mtoto au watoto kwa asilimia 35 yanatoka upande wa wanaume na asilimia 65 ni wanawake, kutokana na tafiti mbalimbali," alisema Prof. Janabi.

"Kwa hospitali yetu MNH kila siku katika wagonjwa 10 tunaowaona kliniki ya kinamama watatu hadi wanne wana tatizo la uzazi. Asilimia 30 ya wagonjwa tunaowaona wana tatizo. Baada ya kuona kuna masononeko katika nyumba zetu, tulifanya maamuzi kununua vifaa vilivyogharimu Sh. bilioni 1.1."

Alisema kwa wanawake ambao kwa sasa hawako tayari kupata watoto aidha kuwa masomoni, wanaweza kuhifadhi mayai yao kituoni hapo na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji huo na kwamba MNH itaendelea kuwaalika wataalamu mbalimbali kutoka nje.

Kuhusu mradi wa gari ya kliniki tembezi ambalo MNH wameipata, alisema usafiri umegharimu dola 200,000 na kwamba hatua hiyo itatimiza utoaji huduma za kuwafikia wananchi pale walipo.

Katika mradi wa upandikizaji vifaa vya usikivu watoto 14, Prof. Janabi alisema idadi hiyo inafikisha waliopandikizwa kufikia 84 na 73 kati yao wakipandikizwa masikio yote mawili na 11 wamepandikizwa sikio la upande mmoja.

"Watoto hawa 14 leo (jana) wanapata fursa ya kusikia kwa mara ya kwanza, katika jamii watoto wa aina hii huadhibiwa kwamba ni watukutu kumbe tatizo ni usikivu.

Tumeanza na hawa 14 kwa gharama ya Sh. milioni 345 na wengine 24 watafuata kupata huduma hii," alisema. Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma ya Afya Kwa Wote inawafikia wananchi wote, ili kuwapunguzia gharama za matibabu ikiwamo ya kibingwa.

# Askofu Mdegella aonya utekaji, mauaji

**Na Francis Godwin,**
IRINGA

ASKOFU Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, Prof. Owdenburg Mdegella, amekemea matukio mauaji na utekaji yanayoendelea nchini na kuonya kuwa vitendo hivyo vinaweza kusababisha machafuko katika jamii.

Amesema Tanzania inapaswa kujifunza kutoka nchi zilizopitia katika hali hiyo ikiwamo jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) ambayo mpaka sasa hali ya amani ni tete.

Prof. Mdegella, akizungumza na mwandishi wa habari hii ofisini kwake, mjini hapa, alisema matukio ya utekaji na mauaji9 yanayoibuka siku hadi siku nchini hali ambayo inatoa viashiria vya machafuko.

Alisema siku zote damu ya mwanadamu ina tabia ya kudai au kulia, hivyo kuendelea kwa matukio kikatili nchini, kutaliathiri taifa la Tanzania. Aliiomba serikali kuangalia namna ya kudhibiti matukio hayo ili kurudisha imani ya Watanzania kwa vyombo vya usalama.

"Yako mauaji ya aina nyingi. Mara usikie watoto wameuawa, mara usikie watoto wamepotea na wamepatikana hawana viungo, mara viongozi fulani wa chama wanakufa kiajabu ajabu. Hapa ninasema kama mtumishi wa Mungu. Nyie mnaijua Congo ndiyo tajiri kwa nchi zote Afrika kwa maliasili, lakini haituli kutokana na damu ya Patrice Lumumba inalia," alisema.

Askofu Prof. Mdegella alishauri viongozi wa juu wa nchi wajaribu kutumia mbinu kali kuwawabana wanaosababisha vifo vya wengine bila sababu yoyote na vyama vya siasa kuachana na fitina za kisisa ili kukomesha mauaji.

Pia aliwataka wananchi wa mkoa wa Iringa kujitafakari upya ili kuona namna ya kuondokana na matukio mabaya yanayoonekana kushamiri zaidi ndani ya mkoa huo.

Alisema mkoa wa Iringa umekuwa na matukio ya kutisha kama vile ubakaji na ulawiti wa watoto, ulevi kupindukia, utapiamlo, kukithiri kwa imani za kishirikina na kuwa juu katika maambukizi ya Ukimwi jambo ambalo halileti taswira nzuri.

"Ninafikiria hata kuomba kibali cha serikali ili kupata nafasi ya kuzungumza mkoa kwa mkoa na hapa Iringa nitasemea Samora ili kukemea mambo haya ambayo yanatia kinyaa. Kila siku tunasikia matukio ya kutisha na mengine yakifanywa na tuliotegemea watulinde. Damu hii inayolia ikiendelea itatugusa hata tusiohusika," alisema.



Askofu mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, Prof. Owdenburg Mdegela, akizungumza mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

Pia aliwakumbusha viongozi wanaoteuliwa kuwa na busara katika uzungumzaji wao ili kujiepusha na uzuaji wa taharuki kwa jamii wanayoiongoza.

"Mtumishi anayeteuliwa anapaswa kujua namna ya kutunza siri na ndiyo maana wanakula viapo," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Askofu Prof. Mdegella, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na utendaji wake kuwa bora na kuongeza kuwa anajua kuna watu watamkosoa lakini kwa umri wake ameona marais wengi wa Afrika na utendaji wao, hivyo anavyompongeza na anatambua anachokisema.

"Mimi nimeangalia viongozi wengi wa Afrika lakini Rais Samia bado ni kiongozi mzuri. Najua watu wanasema anapewa pesa na Waarabu siju nini. Sasa vitu kama hivi ulikuwa wapi wakati anapo pewa pesa hizo," alisema.

# Wamlilia waziri gharama kubwa za matibabu MOI

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wagonjwa wanaopatiwa huduma katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), wamemweleza Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, changamoto wanazokumbana nazo hasa gharama kubwa za matibabu.

Wagonjwa hao, ndugu na jamaa zao, walisema hayo kwa nyakati tofauti jijini Dar es Salaam, baada ya Waziri Mhagama kufanya ziara MOI na kuwataka kutoa madukuduku yao kuhusu huduma hospitalini hapo.

Mmoja wa wananchi hao, Abdallah Shaaban, alisema ili kufanikisha matibabu ya ndugu yake, imempasa kuuza baadhi ya mali kwa ajili ya kulipia gharama za matibabu.

"Mama yangu kalazwa hadi sasa huduma ni Sh. milioni mbili. Nimetoa Sh. 600,000 nimeuza mahindi, mimi ni mkulima. Naomba serikali inione mtu kama mimi napata wapi hela hadi sasa nimeshatoa zaidi ya Sh. milioni mbili," alisema.

Thadei Kivamba alisema anaiomba serikali iwapunguzie wananchi gharama za huduma tofauti, kama vile ya kulaza mgonjwa chumba cha uangalizi maalumu (ICU), inayofikia Sh. 80,000 kwa siku.

"Nimetoka Tosamaganga mkoani Iringa, mgonjwa wangu kitanda kulala ICU ni Sh. 80,000 kwa siku. Kwa Mtanzania wa kawaida, anapata wapi fedha hii? Hapo bado vipimo, dawa na kumwona daktari bingwa," alisema Kivamba.

Amina Baraka, alisema mgonjwa wake kafanyiwa upasuaji wa kichwa gharama hadi sasa imefikia Sh. milioni sita, ikimuwia vigumu kulipa.

"Mgonjwa wangu kafanyiwa upasuaji wa kichwa. Tuliuza vitu nikaja na Sh. milioni tatu na deni ni Sh. milioni nne, bado dawa nimeambiwa Sh. 100,000 jana (juzi)," alilalamika.

Akijibu hoja hizo, Waziri Mhagama alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora, kwa kuchangia gharama kidogo ikilinganishwa na hospitali binafsi.

"Tunasisitiza ni mgonjwa akifika apewe huduma kwanza, mengine yanakuja baadaye. Okoa maisha kwanza ya mgonjwa halafu deni lifuate, tunatarajia kukamilisha kanuni za Bima ya Afya Kwa Wote, ambayo itasaidia kupunguza gharama za matibabu," alisema Mhagama.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Lemeri Mchome, alisema gharama za huduma haziepukiki kwa kuwa fedha zinahitajika kwa ajili ya uendeshaji na kufanyia ukarabati mashine za vipimo vya kisasa.

"Huduma ya afya haitolewi bure kwa sababu kila mmoja anatakiwa kuchangia ili kufanya iwe endelevu. Mfano kufanya upasuaji wa kichwa MOI kwa mgonjwa mmoja ni takribani Sh. 600,000 baadhi ya hospitali binafsi inafikia hata Sh. milioni 20," alisema Dk. Mchome.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: OPERATIONS LOGISTICS COORDINATOR**

**Job Type:** Full Time

**Location:** Marine Storage Terminal, Tanga

**Reports to:** N+1: Head of Logistics | N+2: Operations Director

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

- Manages all aspects of Facilities and General Services for EACOP properties in Tanzania.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**In accordance with policies and procedures in place in EACOP, Operations (Logistics) is responsible for:**

- Manage all facilities' service contracts including but not limited to vehicle maintenance, utility maintenance, housekeeping, domestic waste disposal, catering contracts, etc.
- Be point of contact (interface) for all community landlords within EACOP operational areas.
- Scheduling transportation services including site shuttles within an operational area.
- Manage and monitor inter-site personnel movements especially to unmanned stations.
- Allocating drivers and planning routes.
- Management of diesel inventory at all sites and supply to operational vehicles.
- Periodic site visit for audits, inspections and visual evaluation of operational needs for non-technical materials and interventions.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

**EACOP is committed to ensuring that the health, safety and welfare of workers, communities, and the environment are well addressed and managed. Therefore, the employee is mandated to:**

- Fully comply with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participate in HSEQ and promote this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicate to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintain a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor's degree in business administration, logistics or related field with.

**Experience Required:**

- 5+ years of experience in Logistics operations involving facility management and maintenance.
- Rigor.
- Good communication skills.
- Excellent time management and organizational skills.
- Knowledge of logistics software or transportation management systems.
- Basic accounting knowledge.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 30th September 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: WAREHOUSE & STOCK COORDINATOR**

**Job Type:** Full Time

**Reports to:** N+1: Head of Logistics | N+2: Operations Director

**Location:** Marine Storage Terminal, Tanga

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

- Manages all activities of the various EACOP warehouses at MST (main warehouse), PS-1, PS-4 & PS-5.
- Manage the Warehouses Specific Maintenance Contract (SMC).

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**In accordance with policies and procedures in place in EACOP, The Warehouse & Stock Officer is responsible for:**

- Provide support for inventory management and warehousing activities.
- Reviews material and cargo handling and storage tasks.
- Follow-up of all transport vehicles dispatched to the operational sites.
- Responsible for proper database management for electronic documentation related to material delivery.
- Monitors warehouse inventory levels and place orders as required.
- Provides information to customers (maintenance and operations teams) on the status of their orders.
- Ongoing follow-up with suppliers for out-of-stock goods.
- Continuously tracks inventory at our warehouse, manages receipt and labeling issues with the warehouse supervisor.
- Monitors expected delivery times and identifies any delivery delays to proactively intervene with suppliers to correct the situation.
- Handles products to ensure quality.
- Organize MST main warehouse catalogue goods, plan routes and process shipments.
- Carries out periodic site visits (to PS-1, PS-4 & PS-5) to ensure compliance with approved warehouse management rules and procedures.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

**EACOP is committed to ensuring that the health, safety and welfare of workers, communities, and the environment are well addressed and managed. Therefore, the employee is mandated to:**

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor's degree or Advanced Diploma in one of the following fields: Taxation, Customs, Accountancy, Finance, Economics, Business Administration, Law or equivalent.

**Experience Required:**

- Proficiency in English, both spoken and written.
- Knowledge of the processes used in operational logistics: transportation regulations practices, routes, contacts, best practices.
- 10 years' experience in logistics operations involving warehouse management.
- Adaptability, diplomacy, rigor.
- Compliance with procedures.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 30th September 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (kulia), akitoa maelekezo kwa viongozi wa Bandari ya Dar es Salaam juzi, alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua namna kituo cha mita za kushushia mafuta (flow meter) Kurasini Oil Jet (KOJ) kinavyofanya kazi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa azindua mfumo wa kielektroniki EPZA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua rasmi mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji Kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Mauzo ya Nje (EPZ), ili kutoa urahisi kwa wawekezaji popote walipo duniani kupata taarifa sahihi za uwekezaji nchini na namna ya kujisajili bila ya kufika nchini.

Mfumo huu ulioanzishwa na Mamlaka ya Kanda za Maendeleo ya Uwekezaji (EPZA) ni moja ya utekelezaji wa maagizo ya Raisi Samia Suluhu Hassan ya kutaka taasisi zinazosimamia uwekezaji kuendelea kutengeneza mazingira wezeshi ya kuvutia na kuendeleza uwekezaji nchini.

Uzinduzi huo ni moja ya tukio muhimu wakati wa hafla ya uzinduzi wa taarifa tano za Maboresho ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji na Nyenzo za Usimamizi wa Uwekezaji nchini uliofanyika Septembe 11, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu aliagiza taasisi za serikali na mamlaka kuharakisha marekebisho ya sheria zitakazowezesha shughuli za biashara na kuhakikisha kwamba kanuni mpya zinaimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji.

"Masuala haya yanapaswa kuendana na kuweka kipaumbele katika kutoa huduma kwa haraka, kwa ufanisi, na kwa kufuata viwango vya kimataifa. Mamlaka zinapaswa kuwa na mifumo iliyo rahisi ya mawasiliano na wawekezaji na kuondoa vikwazo vilivyopo," alisema.

Ripoti nyingine zilizozinduliwa ni pamoja na Mwongozo wa Kitaifa wa Maendeleo na Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ), Ripoti ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; Ripoti ya Uwekezaji wa Kitaifa kwa mwaka 2023 na Mpango wa Mkakati wa Ofisi ya Rais, Mpango na Uwekezaji kwa kipindi cha 2024/2025 - 2025/2026.

Pia, aliziagiza taasisi za serikali na mamlaka kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi, kwa kuwa inaweza kutoa maarifa na mapendekezo muhimu kwa maboresho yanayohitajika.

Alisisitiza umuhimu wa mipango ya maendeleo kutoa mafunzo na huduma kwa wadau wa biashara, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya zana mpya za usimamizi wa uwekezaji. Kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji Kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Mauzo ya Nje (EPZ), wawekezaji watashughulikia masuala yao ya uwekezaji kwa haraka na ufanisi, bila kujali mahali walipo.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema kuwa uzinduzi wa mfumo huo mpya ni sehemu ya maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji nchini.

"Huduma hii muhimu inawakilisha hatua nyingine muhimu katika kuendeleza mazingira rafiki ya biashara nchini Tanzania," alisema.

Alisema mfumo utarahisisha mchakato wa uwekezaji kwa kuondoa haja ya wateja kusafiri hadi ofisini kupata huduma.

Sasa wanaweza kujiandikisha mtandaoni, kupata leseni zao, na kupokea vivutio vinavyohitajika kutoka popote walipo.

Uzinduzi wa mfumo huo utaiwezesha Tanzania kushindana vema kuvutia uwekezaji wa kigeni mkubwa nchini. Serikali inatazamia kuvutia uwekezaji wa ndani na wa kigeni, kuhamasisha ajira na kukuza maendeleo ya kiuchumi endelevu.

# TPA yapata tuzo ubora wa huduma

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetunukiwa tuzo ya ushindi wa jumla katika Maonesho ya 19 ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayofanyika katika viwanja vya Furahisha, jijini Mwanza na kushirikisha zaidi ya taasisi 200 kutoka nchi wanachama.

Akizungumza wakati wa kutoa tuzo kwa TPA, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk.

Selemani Jafo, alisema tuzo hiyo ya TPA imetokana na uboreshaji wa huduma katika bandari inazozisimamia kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika.

Waziri Jafo alisema TPA imekuwa mshindi wa kwanza kati ya Taasisi za Serikali zilizoshiriki kwenye maonesho hayo kwa kuwa na banda bora lenye kuvutia zaidi katika maonesho hayo.

"Mafanikio haya ni matokeo ya usimamizi mzuri unaofanywa na TPA ikiwamo uwekezaji unaofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam," alisema.

Maonesho hayo yenye kaulimbiu ya "Uboreshaji wa Mazingira ya Uwekezaji na Biashara ni Kichocheo Katika Kukuza Uchumi wa Nchi" yana lengo la kukuza fursa za biashara na kuzwezesha nchi wanachama wa Afrika Mashariki kuchangamkia fursa ya masoko ya jumuiya nyingine ikiwamo vile SADC.

Akifungua maonesho hayo, Waziri Jafo alisema malengo ya serikali ni kuboresha upatikanaji wa huduma katika sekta mbalimbali zikiwamo miundombinu ya barabara, reli na anga ili kukuza ukuaji wa biashara na uchumi.

Jafo alisema uwekezaji mkubwa umefanyika katika bandari za Dar es Salaam, Mwanza na maeneo mengine ili kurahisisha wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kusafirisha biashara zao kwa haraka na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Akitolea mfano Bandari ya Dar es Salaam, alisema uwekezaji uliofanyika katika bandari hiyo ambayo ni kiungo kikubwa kwa nchi nane zisizo na pwani katika Afrika Mashariki, Kusini na Kati kumeongeza ufanisi mkubwa katika kuhudumia shehena za meli za mizigo zinazotia nanga bandarini hapo.

Bandari ya Dar es Salaam pia ni kiungo muhimu cha usafirishaji wa mizigo kwenda Mashariki ya Kati, Ulaya na hata bara la Amerika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa mamlaka hiyo, Leonard Magomba, alisema mamlaka sasa ina malengo zaidi ya kuboresha bandari zake zingine kupitia upanuzi wa miundombinu, uwekezaji katika vifaa, na kuajiri wataalamu ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya kimataifa vya utoaji huduma.

"Kwa sababu ya uwekezaji huu mkubwa, Bandari ya Dar es Salaam sasa inaweza hata kupokea meli kubwa zenye urefu wa hadi mita 300.

"Hii imewezekana kwa kupanua kina cha lango la kuingia bandarini na eneo la kugeuzia meli, hali inayowezesha meli kubwa kutia nanga kwa urahisi zaidi," alisema Magomba.

# Mfumo wa kuunganisha watoa huduma kifedha waandaliwa

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema imeandaa utaratibu utakaowezesha ushirikiano kati ya benki na watoa huduma za fedha kwa njia ya mtandao ili kuimarisha huduma hiyo nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam kwenye Kongamano la Wafanyabisahara na wawekezaji Afrika Mashariki, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Sauda Msemo, alisema kwa sasa teknolojia inazidi kukua, hivyo ni muhimu kwenda nayo sambamba.

"Huduma hizi za kifedha kwa njia ya mtandao zinazidi kukua na serikali tayari imeandaa utaratibu mzuri kwa pande hizi mbili kushirikiana ili kusaidia kukuza huduma hii," alisema Msemo.

Katibu Mtendaji wa Chama cha Watoa Huduma za Kifedha kwa Njia ya Mtandao (TAFINA), Shedrack Kamenya, alisema malengo makubwa ya kuwakutanisha watoa huduma za kifedha na watunga sera na wadau wengine ni kuangalia namna ya kukuza sekta hiyo pamoja na kuangalia changamoto za wizi wa fedha katika huduma hizo.

"Moto wetu mkubwa ni kuwekeza na kuingia ubia kuhakikisha watu wote wanaingia katika utoaji huduma za kifedha kwa mtandao, lakini pia maeneo tunayoyaangazia ni mazingira ya kifedha kusaidia upatikanaji wa huduma na wizi wa fedha kwa njia ya mtandao," alisema Kamenya.

Pia alisema wizi wa fedha kwa njia ya mtandao ni eneo muhimu ambalo wanaliangazia katika kongamano hilo ili kupata njia ya kudhibiti. Alisema kampuni 10 kutoka nchi mbalimbali zinashiriki katika kongamano hilo la siku mbili.

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo, ambaye ni Meneja wa Soko la Afrika wa kampuni ya G-Payment, Alfred Tembo, alisema TAFINA imeona umuhimu wa kushirikisha nchi za Afrika Mashariki katika kukuza sekta hiyo nchini.

"Lakini pia nipongeze utayari wa serikali ya Tanzania katika kupokea wawekezaji hasa kwenye sekta hii ili kurahisisha ulipaji fedha katika huduma mbalimbali," alisema Tembo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaotumia mitandao vibaya wadhibitiwe

**MAPAMBANO** dhidi ya uhalifu mitandaoni ni jambo muhimu hasa wakati dunia ikiwa kwenye mabadiliko ya kutumia teknolojia ya mawasiliano.

Kuna mambo mengi yanayotokea katika kipindi hiki huku wahalifu wakitafuta mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanakwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Dunia kwenda na mabadiliko ya teknolojia ni kurahisisha kazi na kupunguza muda unaotumika kwa binadamu kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, kuna watu wanaotumia fursa hiyo kujinufaisha na kuona hawaachwi nyuma kwa jambo lolote lile.

Kuna watu wanaotumia teknolojia hiyo kuandika mambo ya uongo kwa kutumia jina la kampuni fulani ionekane kama ndio iliyofanya jambo hilo.

Ndio maana kuna umuhimu wa kuhakikisha kama jambo hilo ni sahihi kutoka kwenye kampuni husika kabla ya kuanza kuishambulia.

Pia, wapo wanaotumia picha za matukio ya zamani na kuzitengeneza ili mradi kuwachafua watu na kuwaharibia wasifu wao. Teknolojia hii isitumike kuharibu badala yake watu waitumie kujifunza mambo yenye maendeleo kwa faida yao na taifa.

Miaka ya nyuma kabla ya teknolojia ya mawasiliano haijabadilika, kazi nyingi zilikuwa zikifanyika kwa kwenda sehemu husika, lakini sasa hivi mtu anaweza kukaa nyumbani na akamaliza kila kitu kwa kutumia simu yake ya mkononi.

Siku za nyuma sehemu zenye huduma muhimu kama ulipaji wa bili za umeme, maji na benki, mtu ilibidi aende kwenye ofisi hizo hali iliyokuwa ikisababisha msongamo mkubwa wa watu.

Sasa hivi hata ukiwa nje ya nchi unaweza kufanya miamala na kulipia bili zako kwa wakati.

Kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi ilikuwa inachukua muda kumtumia ndugu yake pesa, lakini kwa sasa teknolojia imerahisisha, hakuna usumbufu tena.

Lakini, teknolojia hiyo imeingiliwa na kutumika vibaya kwa baadhi ya wahalifu kwenye sekta ya fedha kwa kuwaibia watumiaji na kuwafanya waogope kuitumia.

Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), imeeleza wazi kuwa inaendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti uhalifu mitandaoni, ikiwamo huduma za kifedha kutokana na kuongezeka mifumo mipya ya mawasiliano ya teknolojia.

Inapokuja teknolojia mpya ni muhimu ikatumika vizuri ili kunufaisha watu na kuondoa ugumu uliokuwapo mwanzo.

Kwa nchini Tanzania, wafanyabiashara, wajasiriamali wamerahisishiwa kazi kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ambapo kwa sasa wanaweza kutuma pesa nje ya nchi na kuletewa bidhaa wanazotaka badala ya kusafiri hali inayowapunguzia gharama.

Katika matumizi ya teknolojia hii pia kunahitajika uaminifu wa hali ya juu ndio maana hata TCRA ikiwa ni mdhibiti wa matumizi mabaya ya mawasiliano imekuwa ikiingilia kati kila inapoona mambo hayaendi sawa.


Kuna wanaotumia teknolojia hiyo pia kwa malengo mabaya ya kuwachafua watu wengine kwenye mitandao.

Hali hiyo imekuwa ikishamiri kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuharibu hali ya hewa na wengine wanaochafuliwa huathirika kisaikolojia.

Viongozi wa juu wanapokuwa kwenye majukwaa wamekuwa wakikemea tabia hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa kama isipodhibitiwa itarudisha nyuma maendeleo.

Duniani mabadiliko ya kiteknolojia hayawezi kuepukika, hivyo ni muhimu wadhibiti wa uhalifu mitandaoni kuwa makini kudhibiti hali hiyo ili kuepuka matumizi mabaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vijana wenzangu, tuwe wenye busara katika kusimamia kanuni za mapenzi

Na Tuntule Swebe

**NI** jambo la kawaida sana, maisha na uhusiano au ndoa na uhusiano kuwa mzuri, pale wawili wanaporidhiana. Vilevile, pale yanapoingia doa, ndio panapogeuka kuwa tatizo.

Kwani kuna baadhi ya watu, waliokuwa kwenye uhusiano, huangukia kwenye kusaliti wenzi wao, wakaibuka na ama wanaume au wanawake wengine.

Mtu anayetendewa hivyo pindi anapogundua mwenza wake, anamsaliti huwa anumia na hapo ndipo fikra mpya zinajitokeza na akawa anaonekana kuwa na mtazamo hasi.

Huwa wanapokumbwa na tatizo hilo, inawalazimu kuwa wakali kupita kiasi na hata wanashindwa kudhibiti hasira. Wanamaliza maumivu yao kwa watu tofauti na waliowakosea.

Katika hilo, kuna wengine wanaofikiria hatua ya kujiua. Wanaofanya hivyo wako katika matazamo walichotakiwa ni kulitatua tatizo hilo, kupitia namna hiyo. Lakini, jibu linabaki kwamba, hiyo haikuwa sahihi, kwani ina hasara.

Tumeona watu wengine wakiwa na upweke, huku baadhi yao wanakosa hasara ya kupoteza wapendwa wao, walioumbwa na matatizo ya namna hiyo.

Sambamba nao, wapo wanaopata matatizo ya afya ya akili, kwa sababu tu ya hilo la mvurugano kimapenzi, wakifikia hatua ya kuongea peke yao na baadhi ya hatua isiyo sahihi kibinadamu.

Chanzo kinabaki kuwa mapenzi. Hivyo, tukibaki pasipo kulitafakari hilo, ni kwetu jamii tunapoteza mwelekeo na kwa tafsiri pana tunaunda taifa tegemezi.

Nakumbuka hadithi, kulikuwapo watu wawili wanaosadikiwa kuwa ni wapenzi Katalina Juma (21) na Athanas Alyen (23) wakazi wa mkoani Katavi, wamekutwa wakiwa wameuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali, huku chanzo kikitwa wivu wa mapenzi.

Tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia Oktoba 19, mwaka jana, ambapo marehemu wote wakakutwa wamefariki dunia kwa kuchinjwa na kutupwa pembezoni mwa barabara.

Mwenyekiti husika akakaririwa, amesema marehemu hao walikutwa na madhila wakiwa wanarudi nyumbani, kutokea kijiji chao kiitwacho Kabungu, walikokuwa wakifanyia shughuli zao.

Akithibitisha kutokea tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, , akasema wanawashikilia watu wawili kuhojiwa, huku akieleza kuwa tukio hilo lina sura ya 'wivu wa kimapenzi', kwa kuwa wamebaini mmoja wa marehemu alikuwa akiwasiliana na watu ambao walikuwa wapenzi wake.

Kamanda huyo akaahidi kuwa Polisi inaendelea na upelelezi wa tukio hilo na mara utakapokamilika, watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani.

Pia, kuna taarifa nyingine ya mwanafunzi wa chuo kikuu, ambaye jina lake halikuwekwa wazi, akaadaiwa kutaka kufanya jaribio la kujiua akiwa chuoni hapo. Chanzo kinatajwa ni masuala ya mapenzi.

Ni tukio la Aprili 25, 2024 wakati alipokuwa katika moja ya majengo ya chuoni kwao na taarifa za awali, zikaeleza kuwa alipokorofishana na mpenzi wake, alitaka kujirusha kutoka juu ya ghorofa ya nne.

Ikaatarifiwa baadaye alikuwa amelazwa hosptalini, baada ya kuonekana hakuwa sawa.

Ujumla wa hali halisi hiyo, ni kwamba kuna haja ya elimu ya kina isambazwe baina ya wahusika wakifanya mazoezi ya Pamoja, wanashirikiana na marafiki zao ili kuweza kusaidia mfumo wa afya ya akili iende inavyopaswa, hali yenye msaada kwa kiasi kikubwa katika maisha ya jamii. Bila shaka, walio kwenye uhusiano wa kimapzi watazingatia haya yanayowahusu.

Hata hivyo, kwa wale waliopoteza wapenzi walioondoka katika maisha ya duniani, inawapasa wasikate tamaa, waanze upya ulikukabiliana na hili uaminifu ni bora zaidi.

## HABARI KITAIFA



Ofisa Habari na Uhusiano wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Said Ameir, akitoa elimu ya takwimu kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi adaiwa kumshushia kipigo mwalimu

**Na Halfani Chusi**

Askari Polisi wa Kituo cha Polisi Chamwino, Herry Sanga, anadaiwa kumshushia kipigo Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Chamwino mkoani Dodoma, Dominic Sullumo, baada ya kumfuata akiwa kazini kwake.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Alhamisi iliyopita majira ya asubuhi, hivyo kumsababishia mwalimu huyo maumivu sehemu mbalimbali za mwili wake yaliyolazimu alazwe hospitalini kwa uangalizi.

Mkuu wa Mkoa Dodoma, Rosemary Senyamule, alithibitisha juzi kuwapo kwa tukio hilo na kusema kulikuwa na ugomvi baina ya askari na mwalimu na kwamba hafahamu chanzo cha mgomvi wao.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi juzi kwa simu, Senyamule alisema anafahamu kutokea kwa tukio hilo na kwamba mwalimu alikimbizwa hospitali kwa ajili ya matibabu.

"Ninafahamu pia huyo polisi anashughuliwa katika ngazi zao za kipolisi, tangu mwanzo ninajua hatua hizo zimechukuliwa japo bado sijafuatilia kujua maendeleo ya mgonjwa kwa sasa.

"Sheria inakataza kupigana kosa hilo lina adhabu yake unaweza kufukuzwa kazi au kupewa adhabu nyingine zilizotajwa kwenye sheria," alisema.

Senyamule alisema ni muhimu pale unapojiona unakaribia kupata hasira kuchukua hatua za kujizuia, ikiwamo kuwaona viongozi wa dini au watu wa ushauri nasaha badala ya kuchukua sheria mkononi.

Aidha, aliwataka wananchi katika mkoa wake wanapokosewa wasijichukulie sheria mkononi baadala yake wafike katika vyombo husika kwa usuluhishi.

Alipotafutwa kwa ajili ya ufafanuzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, alisema: "Hii taarifa mbona vyombo vya habari vilisharipoti njoo ofisini kesho asubuhi mimi nipo Kondoa kwa sasa."

Hata hivyo, mwandishi wa habari hizi alivyomwambia kuwa yuko nje ya Dodoma, Kamanda huyo alisisitiza apigiwe simu leo asubuhi.

**ILIVYOKUWA**

Akisimulia mkasa huo, mmoja wa walimu katika shule hiyo ambaye hakutaka jina litajwe gazetini, alisema siku ya tukio askari huyo akiwa amevalia suti alifika shuleni hapo na kuomba kuonana na mkuu wa shule.

"Baada ya kuonana naye akamwomba wakazungumzie ofisini kwake kwa sababu anamfahamu kuwa ni mume (Askari) wa mwalimu wake shuleni hapo alikubali na alikuwa haoneshi dalili zozote mbaya.

"Wakati wanakwenda ofisini mkuu wa shule alikuwa ametangulia mbele wanavyokaribia mlangoni kwenye ofisi yake akiwa kwa nyuma akampiga ngumi kwenye mshipa wa shingo akadondokea kwenye kochi.

"Akamuwahi kabla hajanyanyuka akaanza kumshambulia baadaye walimu wengine wakashtuka kama kuna ugomvi unaendelea ndio wakakimbia kwenda kuamulia, lakini mpaka wanafika alikuwa tayari ameshamuumiza vibaya sana," alisema mwalimu huyo.

Alisema siku hiyo kulikuwa na semina iliyokuwa inaendelea shuleni hapo, alikuwapo pia Ofisa Utumishi ambaye alishuhudia tukio hilo na alirekodi baadhi ya picha na video.

"Basi baada ya hapo watu walijaa na kuwaamulia kugombelezea na wanafunzi wanataka kuingilia ikabidi yule askari atolewe ndio pakatulia.

"Aliumizwa zaidi sehemu za usoni na upande mmoja wa jicho ulikuwa umevimba bahati nzuri akaja Mkurugenzi wa Halmashauri, Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) na maofisa wengine kutoka serikali wakachukua picha walivyomaliza wakaondoka wakati tayari mkuu wa shule amekimbizwa hospitalini," alisema.

Akitolea ufafanuzi suala hilo katika chombo cha habari mtandaoni, haki TV kuhusiana na tukio hilo Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Tito Mganwa, alisema: "Tulipata taarifa za fujo na uvunjifu wa amani katika shule hiyo tulitoa taarifa Kituo cha Polisi Chamwino na suala hili linaendelea kufanyiwa uchunguzi na Jeshi la Polisi.

"Kwa sababu ni suala la kiuchunguzi ninaliachia Jeshi la Polisi, kwa sababu lenyewe ndio linahusika na suala hilo, lakini kwa sasa shuleni amani ipo na shughuli zinaendelea kama kawaida," alisema.

Aidha, alionya kwamba shuleni ni mahali pa kutolea elimu na malezi hapahitaji ghasia wala fujo na hivyo wanaposikia kuna hali hiyo bila kujalia nani mhusika cha kwanza wanahakikisha usalama, lakini kama kutakuwa na uhalifu sheria lazima ichukue mkondo wake.

Alisema kwa sasa mkuu huyo na anawasiliana naye muda wote na tayari yuko nyumbani kwake anaendelea vizuri.

Vyanzo mbalimbali vimelieleza gazeti hili kuwa chanzo cha ugomvi huo kimetokana na madai kwamba mkuu wa shule huyo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mke wa askari huyo ambaye anafundisha katika shule hiyo.

Hata hivyo, chanzo hicho kimeeleza zaidi wakati askari huyo akitembeza kipigo hicho alikuwa akitamka "Nitakuua mimi kwa nini unatembea na mke wangu nitakuua."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alisema ikithibitika kama kweli walipigana jambo hilo litakuwa halina picha nzuri kwa watumishi wa umma.

Alisema watumishi wa umma wana maadili yao ikiwamo kuwa mfano bora kwa jamii kuishi kwa heshima na kama itathibitika hivyo ni kitu cha kusikitisha na ni jambo linaloitia aibu serikali.

"Kwa mujibu wa sheria haitakiwi mtu yoyote kupigwa hata kama ni kweli alitakiwa atoe taarifa katika kituo kingine cha polisi ambacho hatokuwa na masilahi nacho na asimame kama raia wa kawaida," alisema Dk. Anna huku akilitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi ili haki itendeke.

# RC akemea biashara usafirishaji binadamu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amekemea usafirishaji haramu wa binadamu hususani wenye ulemavu ambao wanakwenda kutumikishwa kama mitaji ya kuombea fedha.

Alikemea hayo juzi wakati akifungua Kongamano la Wanawake Kanda ya Afrika Mashariki na Kati wa Kanisa la Waadventista Wasabato linalofanyika eneo la Ititi, Manispaa ya Singida na kushirikisha zaidi ya wanawake 2,000 kutoka nchi 11.

"Niwaombe wanawake tusimame imara kulikemea hili kwani tukijisahau linaweza kushamiri na kujikuta katika jamii zetu tunasababishiana ulemavu wa makusudi," alisema.

Dendego aliwakumbusha wanawake kutimiza kikamilifu jukumu la wazazi na walezi kwa kusimamia vyema maadili ya watoto wa kike na wa kiume.

"Sote tumekuwa mashuhuda wa athari zinazotokana na kumomonyoka kwa maadili kunakopelekea kuibuka kwa vitendo ambavyo ni kinyume cha mila, desturi na utamaduni wa kiafrika," alisema.

Alisema kila mmoja kwa nafasi yake ahakikishe anakemea na kupinga vitendo vya uhusiano wa jinsia moja kwa kuwa suala hili linaumiza jamii, linapoteza nguvu kazi ya taifa na ni haramu katika imani ya dini zote na dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Dendego alilipongeza Kanisa la Waadventista Wasabato kwa kujenga kituo ambacho kitakuwa kinasaidia kutoa mafunzo ya stadi za kazi waraibu wa dawa za kulevya, watoto wa mitaa na makahaba ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Kituo hicho ambacho ujenzi wake unaendelea, kinajengwa na kanisa hilo kupitia dara ya wanawake kwa fedha zinazochangwa na wanawake kutoka nchi 11.

"Binafsi ninawapongeza sana kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa mwanamke katika jamii kwa kuwapa fursa ya kumtumikia Mungu na kuzisaidia jamii zetu," alisema.

Alisema ni ukweli mtu kuwa Mungu amewapa wanawake uwezo mkubwa na iwapo watatumia fursa kikamilifu familia, jamii, taifa na mataifa yatastawi kutokana na uwezo na vipawa vya kipekee ambavyo Mungu amewapa wanawake.

"Hapa kwetu Tanzania kuna usemi usemao wanawake wakiwezeshwa wanaweza, ninataka wanawake wenzangu tutoke kwenye kifungo cha usemi huu hatuhitaji kuwezeshwa bali tunapaswa kujiamini kuzitambua fursa na kuweka jitihada zetu sisi wenyewe ili kuzitumia kwa manufaa yetu,jamii nanl taifa kwa ujumla," alisema.

Alisema kuwa wanawake ndiyo chanzo cha jamii na walezi wa watoto na wanaume hivyo hakuna mafanikio katika jamii wala kwa mwanaume bila uwepo wa mwanamke imara nyuma yake.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**



# Jafo akemea uchakachuaji vipimo

**Na Mwandishi Wetu,**

MWANZA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameonya tabia ya baadhi ya watu kuchezea vipimo na kuwahimiza wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo kila wanapofanya ununuzi na kuuza bidhaa.

Jafo aliyasema hayo juzi wakati akifungua rasmi Maonesho ya 19 ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayofanyika katika Uwanja wa Furahisha jijini hapo.

"Wizi wa kuchezea vipimo ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na hata vitabu vya dini vinakataza wizi wa vipimo," alisisitiza.

Akizungumzia ushiriki wa Wakala wa Vipimo (WMA) katika maonesho hayo, Ofisa Vipimo Mwandamizi Mkoa wa Mwanza, Lazaro Joram, alisema ni mwendelezo wa utoaji elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa wafanyabiashara mkoani hapa na nchi jirani.

"WMA tunatumia maonesho haya ili kuwawezesha wadau wetu kutambua majukumu yetu, kueleza umuhimu wa kuhakiki na kutumia vipimo sahihi na kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya matumizi ya vipimo. Pia tunaendelea kuwaelimisha kuhusu aina za vipimo vinavyopaswa kutumika katika biashara," alisema.

Joram aliwakaribisha wananchi kutembelea banda la WMA ili kufahamu aina za mizani wanayoweza kutumia katika sekta za kilimo, uvuvi, biashara na usafirishaji.

"Tunazo aina nyingi za mizani lakini si kila mzani unaruhusiwa kutumika katika biashara au katika sekta ya kilimo, hivyo ukitembelea banda letu utakupa elimu ya kutambua mizani sahihi iliyohakikiwa pamoja na kutambua alama zinazowekwa katika vipimo vilivyohakikiwa," alisema.

Kuhusu elimu inayotolewa kwa wananchi wanaotembelea banda la WMA, Joram alisema eneo mojawapo ni kuhusu namna sahihi ya ufungashaji wa mazao ya shamba. Kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, mazao yote yanatakiwa kufungashwa kwa uzito usiozidi kilo 100 na endapo mkulima atafungasha kwa uzito zaidi ya uliotajwa kisheria, atakuwa amefungasha Lumbesa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Kwa sasa tafsiri ya lumbesa ni uzito unaozidi kilo 100 tofauti na awali ilivyokuwa inatafsiriwa kama kuongeza kifungashio juu ya gunia, hivyo tunawahimiza wakulima kutumia mizani ili kujua uzito wa mazao wanayofungasha," alisisitiza.

Alisema katika Kanda ya Ziwa kuna mazao ya kimkakati ya pamba na kahawa na kwamba ni jukumu la WMA ni kuhakiki mizani yote inayotarajiwa kutumika kwenye ununuzi wa mazao hayo kabla ya msimu kuanza.

Jioram alisema baada ya kufanya uhakiki, mizani iliyo sahihi huruhusiwa kutumika katika ununuzi wa mazao hayo.

Pia alisema wakati wa ununuzi, WMA hufanya ukaguzi wa kushtukiza katika Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) ili kujiridhisha kama mizani inatumika kwa usahihi kama ilivyohakikiwa ili kuwalinda wakulima.

Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa WMA anayeshiriki maonesho hayo, Paulus Oluochi, alitoa wito kwa wananchi kutembelea banda la WMA ili kujifunza kuhusu matumizi sahihi ya vipimo lakini pia kuwasilisha changamoto mbalimbali kama zipo ili ziweze kupatiwa ufumbuzi.

Alisema endapo mwananchi yupo mbali, anaweza kuwasiliana na WMA kupitia nambari isiyo na malipo 0800 110097.

Maonesho ya 19 ya Biashara ya Afrika Mashariki yanatarajiwa kufikia tamati Septemba 15, mwaka huu.




Ofisa Vipimo Mwandamizi wa Wakala wa Vipimo (WMA), Lazaro Joram (kushoto), akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa wadau katika maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki, kwenye viwanja vya Furahisha, jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Megawati zote bwawa la Nyerere kukamilika mwakani

**Na Joseph Mwendapole**

WAKATI mitambo mitatu ya bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP) ikiwa imewashwa na kuzalisha Megawati 705, mitambo mingine miwili imewashwa na inaendelea kufanyiwa majaribio ili ianze kuingiza umeme kwenye gridi ya taifa.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na serikali jana, mitambo yote tisa itakuwa imewashwa na kuanza kuzalisha umeme wa megawati 2,115 kufikia mwanzoni mwa mwakani.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alisema hayo jana wakati akizungumza na wajumbe Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) waliotembelea mradi huo.

Kamati hiyo ilitembelea bwawa hilo jana kuangalia maendeleo ya uwekezaji wa serikali uliogharimu Sh. trilioni 6.5 ambapo mpaka kukamilika kwake bwawa litakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115.

Dk. Mataragio alisema wakati mitambo mingine miwili ikiwa imewashwa na ikiendelea na majaribio, mtambo mwingine mmoja unatarajiwa kuwashwa mwezi Novemba.

"Mpaka sasa mitambo mitatu imeshaanza kufanya kazi katika mradi huo mashine namba 9, 8 na namba 7 ambazo zimeshaongeza umeme wa megawati 705 kwenye gridi ya taifa. Mashine zingine mbili tayari ziko kwenye majaribio na mashine namba tano itawashwa Novemba na mashine namba tatu itawashwa mwanzoni mwa mwaka 2025 na kuzalisha jumla ya megawati 2,115," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa kamati, Marry Masanja, alisema uwekezaji uliofanywa na serikali kwenye mradi huo ni wenye tija kwa kuwa umeleta ongezeko la umeme wa kutosha kwenye gridi ya taifa na kutoa fursa kwa Watanzania kupata ajira mbalimbali katika mradi wakati wa utekelezaji wa ujenzi. "Serikali imewekeza Sh. trilioni 6.5, fedha za Watanzania ili kujenga mradi huu na mpaka sasa Sh. trilioni 6.1 zimeshalipwa kwa mkandarasi na mara mradi utakapokamilika tutakuwa na umeme mwingi zaidi, hivyo tutauza umeme katika nchi za jirani," alisema Masanja

Alisema kamati hiyo inayosimamia masuala ya uwekezaji wa serikali imeridhishwa na uwekezaji uliofanywa katika mradi huo na aliitaka serikali kuendelea kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kimkakati.

"Nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hasan, amesimamia mradi huu mkubwa wa kimkakati na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wake na leo hii umefikia asilimia 98.99. ni mradi wa kujivunia kwa kila Mtanzania," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Nicholaus Ngassa, ambaye pia ni Mbunge wa Igunga, alisema kupitia mradi wa JNHPP hali ya umeme imeimarika nchini na katika jimbo lake wananchi wengi tayari wameunganishwa na huduma ya umeme.

"Hali ya umeme inaendelea kuimarika. Katika jimbo la Igunga, wananchi wengi wana umeme. Nitoe rai kwa wananchi wa Igunga na maeneo mengine tuutumie umeme huu kwa faida yetu hasa katika kutunza mazingira kwa kuanza kutumia umeme kama nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, " alisema Ngassa.

# DED akagua masoko usiku

**Na Steven William,**
MUHEZA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, amefanya ziara ya kushtukiza usiku kukagua usafi katika masoko ya mboga na vyakula mjini hapa.

Dk. Mhina alifanya ziara hiyo juzi katika soko kuu la mboga na soko kuu la vyakula na kutoa maagizo kwa wenyeviti wa masoko hayo na Mkurugenzi wa Mji Mdogo wa Muheza, Johan Mtango, kusimamia usafi kwa wafanyabishara walioko katika masoko hayo.

Alisema anatoa agizo kila Jumamosi wafanyabiashara wote wafungue maduka yao saa 3:00 asubuhi baada ya kufanya usafi wa mazingira katika sehemu zao za biashara.

Alisema atakayekaidi kufanya usafi katika sehemu yake, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupigwa faini. Alisisitiza kuwa, ukaguzi wa usafi katika masoko hayo ni wa kudumu na atakayekaidi usafi atachukuliwa hatua.

Mkurugenzi huyo alisema wafanyabiashara wa masoko hayo wanapaswa kuzoa takataka maeneo yao ya biashara na kuzirundika katika eneo maalum na baadaye litapita gari la mzabuni wa kuzoa taka na kuzipeleka dampo.

Mwenyekiti wa soko kuu la mboga, Hamisi Ally, alisema atahakikisha soko hilo linakuwa safi na mfanyabiashara ambaye atakayekaidi kufanya usafi atachukuliwa hatua.

Mdhibiti Taka wa Halmashauri ya Muheza, Abubakary Iyulu, alisema wataendelea kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo mote ya Wilaya ya Muheza.

Ofisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Siwema Salum, alisema kitengo cha habari kinaendelea kuwaelimisha wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo wanayoishi na ya biashara.

# Matumizi ya ardhi kikwazo uendelezaji zao la kahawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema sekta ya kahawa inakabiliwa na changamoto ya matumizi ya ardhi ya kilimo cha zao hilo katika mikoa ya Kaskazini mwa Kilimanjaro na Arusha.

Mikoa hiyo inatishiwa na kasi ya ujenzi wa makazi na shughuli za utalii, ambazo zinasababisha kushuka kwa kiwango cha uzalishaji.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema hayo wakati akizungumza na wadau wa sekta ya kahawa wakati wa uzinduzi wa Maonesho ya Tano la Tamasha la Kahawa.

Alisema hali hiyo imesababisha kuwapo na tija ndogo ya uzalishaji kwa sasa, ambao umefikia wastani wa uzalishaji wa miti gramu 350, badala ya kilo moja mpaka mbili, ambayo mti wa kahawa unaweza kuzalisha.

Babu alisema watu wameanza kubadilisha maeneo ya kahawa wanajenga nyumba na kuwekeza kwenye utalii.

"Sasa wito wangu, nyumba wakajenge tambarare, mlimani ambako kunastawi kahawa, tuache tulime kahawa. Nimeambiwa tulikuwa tunazalisha tani 25 za kahawa, lakini wakati nimekuja mimi Kilimanjaro, ukaniambia mpaka tani 3,000. Kwa nini, kwa sababu watu walikuwa wanaona kahawa haina faida tena, kahawa bei yake ilikuwa iko chini sana," alisema.

**"Sasa wito wangu, nyumba wakajenge tambarare, mlimani ambako kunastawi kahawa, tuache tulime kahawa. Nimeambiwa tulikuwa tunazalisha tani 25 za kahawa..."**

Zaidi alisema: "Kwa sababu ardhi ya Kilimanjaro ni ndogo, watu wanagawana viamba, watoto hawaendi kutafuta ardhi yake anataka hiyo hiyo. Sasa mimi nataka niseme hivi kama wanataka kujenga nyumba, waende wakajenge maeneo ya tambarare."

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Primus Kimaryo, alisema licha ya Tanzania kulima kahawa zaidi ya asilimia 93 inayokwenda nje, unywaji wetu bado unasuasua kwa asilimia saba.

Alisema kaya 400,000 Tanzania zinalima kahawa, huku asilimia 90 ya wazalishaji wa kahawa wakiwa ni wakulima wadogo, kwamba Tanzania inategemea uzalishaji wa zao hilo katika hekta 220 zilizoko mikoa 17.

Kimaryo alisema: "Ukipita leo hotelini kote wanakolala wageni licha ya Tanzania kuwa mzalishaji mzuri sana wa kahawa, bado kahawa inayonywewa na wageni haitoi taswira kwamba tunatengeneza kahawa nzuri kiasi hicho".

Awali, Mwenyekiti wa wadau na tamasha hilo, Denis Mahulu, alisema wanatamani unywaji wa kahawa ufike asilimia 15 kutoka asilimia saba ya sasa.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (katikati), akizungumza katika kikao cha wazee wa kimila, mjini Musoma jana, kujadili mambo mbalimbali yakiwamo ya kuimarisha maadili mema. Kulia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Taifa, Maganya Fadhili na Mwenyekiti wa Machifu mkoa huo, Chifu Deus Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tamko la EU ununuzi wa kahawa lawaamsha wadau

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MJADALA wa kitaifa kuhusu kanuni mpya za Soko la Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, unaotaka kahawa inayokwenda nchi wanachama wa jumuiya hiyo, yasitokane na uharibifu wa mazingira umeteka hisia za wadau na wakulima kutokana na idadi kubwa ya kundi hilo kujitokeza kushiriki.

Oktoba 4 hadi 6 mwaka huu, wadau na wakulima watajadili kwa kina, mahitaji ya soko la ulaya na dunia inahitaji kitu gani kupitia EUDR kuhusu masoko, ili Tanzania iendelee kuwa sehemu ya soko hilo.

Jana, Mwenyekiti wa wadau wa maonesho ya Kahawa Festival, Denis Mahulu alisema: "Kwa hiyo, tutakuwa na mada kuhusu hilo, wakulima pamoja na wadau mbalimbali watapata fursa ya kushiriki mada hiyo na kuuliza maswali mbalimbali. Vilevile, kuna suala la matumizi ya pembejeo, matokeo ya utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI)."

Wakati jambo hilo la kikanuni likiwaumiza vichwa wadau na wakulima, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alieleza kufurahishwa kwake na kupanda kwa bei ya kahawa.

Babu alisema: "Kilo moja ya kahawa sasa hivi ni shilingi 10,000 kwa kilo moja; na ule mti unatoa mpaka kilo sita. Ukitoa sita maana yake kila mti mmoja wa kahawa unapata 60,000.

Alisema: "Sasa kama una miche 200, kwa hiyo ndugu zangu hapa leo mmekuja watu wa maana sana ambao kwa kweli mmedhamiria kwamba tunataka jambo letu la kahawa festival mwaka huu lisikike dunia nzima".

Aliongeza: "Na habari ya watu kutunyang'anya vitu hapa Kilimanjaro kuvipeleka kwingine sisi tuseme hapana, kuna wenyewe na wenyewe ndiyo sisi au mnasemaje? Basi tukiwaachia tukilegalega watachukua na hii watakwenda nayo".

Aidha, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema vyombo vya usalama, vimemkamata mtu mmoja akiwa na pembejeo za ruzuku anachukua ya Tanzania na kuweka kwenye mifuko ya Kenya, kitu ambacho hakikubaliki.

Babu alisema: "Tunafanya hivyo, serikali ili kuwasaidia wakulima waendelee kuinuka wasiendelee kudidimia. Sasa TCB (Bodi ya Kahawa Tanzania), tusaidieni na mimi niko kwa ajili ya kusaidiana na ninyi kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanazalisha vizuri, maofisa ugani tumewawezesha tumewapa pikipiki na wale wa wilaya wana magari kwenda kuwatembelea wakulima wa kahawa".

# Ujenzi wa stendi, barabara Manyara kuanza mwakani

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, imesema ujenzi wa stendi kuu ya mabasi na barabara za mitaa kwa kiwango cha lami, zenye urefu wa kilometa 7.5 na mitaro kilometa nane, utaanza kujengwa rasmi Januari mwakani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Shaaban Mpendu, aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na mradi wa ujenzi wa stendi kuu ya mabasi.

Alisema halmashauri hiyo ni miongoni mwa halmashauri zilizoingia kwenye mradi wa uboreshaji wa Halmashauri za Miji na Majiji (TACTICS).

"Sisi tutajengewa stendi kuu ya mabasi na barabara za mitaa za lami kilometa 7.5 na mitaro kilometa nane mradi uko hatua za mwisho za usanifu," alisema Mpendu.

Aliyataja manufaa ambayo wananchi watayapata baada ya ujenzi wa mradi huo kuwa ni barabara zitapitika wakati wote, mapato yataongezeka, ajira zitaongezeka na shughuli za kiuchumi zitaimarika.

Alipoulizwa licha ya serikali kuweka mipango ya ujenzi wa stendi kuu ya mabasi eneo la Makatanini na uboreshaji wa miundombinu ya barabara za mitaa kasi ya ujenzi wa nyumba za kuishi watu binafsi bado ni ndogo, alijibu kuwa mazingira yatawafanya wananchi wajenge nyumba zao haraka.

Aidha, alisema kwa watu waliopewa viwanja na wakashindwa kuviendeleza ipo sheria ya kuwachukulia ikiwamo kuwanyang'anya.

Kuhusu gharama zitakazotumika kujenga stendi kuu hiyo na miundombinu ya barabara na ujenzi wa mitaro alieleza kuwa, hawezi kuitaja kwa sasa kwa kuwa zipo hatua zinaendelea.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu ujenzi wa stendi hiyo, mkazi wa Babati, John Sarwath alisema serikali imechelewa kujenga stendi hiyo ambayo inaendana na hadhi ya mkoa.

Mkazi mwingine Yulitha Charles alisema serikali ikijenga stendi hiyo itaongeza idadi ya wafanyabiashara ambao hawajaanza kufanya biashara katika eneo hilo.

Mkazi wa Kijiji cha Kiongozi, Paul Zacharia alisema ujenzi wa stendi hiyo wanausubiri kwa hamu kwa kuwa itawasaidia kuwaletea maendeleo ya haraka.







Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John, akitoa elimu ya kukabiliana na ugonjwa wa kiharusi kwa watumishi wa afya hospitalini hapo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali yawaita wananchi kushiriki uchaguzi S/mitaa

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI mkoani Kigoma pamoja na Msalala wilayani Kahama imewataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika uboreshaji wa taarifa zao kwenye Daftari la Makazi, ili washiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Wito huo umetolewa juzi na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Aman Kanguye, wakati akizungumza na wananchi wa wilayani Kakonko.

Alisema wananchi wanatakiwa kutofautisha taratibu za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Aliwataka kujitokeza kwa wingi katika vituo vya kujiandikisha ili koboresha taarifa zao kwenye Daftari la Makazi, mchakato utakaoanza Oktoba 11 hadi 22, mwaka huu, huku akiwataka viongozi kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi kutofautisha aina hizo za uchaguzi.

Mkuu wa Wilaya ya Kakonko, Kanali Evance Mallasa, alisema serikali wilayani humo itaweka utaratibu mzuri wa kutoa elimu kwa jamii ili watambue tofauti ya chaguzi hizo mbili.

Hata hivyo aliwatahadharisha wale wote wanaotambua kuwa siyo raia wa Tanzania kutojipenyeza kwenye uandikishwaji wa Daftari la Makazi na kwamba atakaye bainika sheria itachukua mkondo wake.

Akizungumza kwenye kikao cha madiwani wa halmashauri hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri, Ndaki Stephano, alisema wananchi wanapaswa kutumia fursa hiyo kutimiza haki yao kikatiba, kuwachagua viongozi wanao wahitaji katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na ule mkuu hapo mwakani.

**Alisema kila mwananchi anawajibu wa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo kwa kujiandikisha kwenye Daftari la Mpigakura au kurekebisha taarifa zake, ili kutopoteza...**

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Rose Manumba alitumia mashindano ya Mahona Cup 2024 kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Alibainisha hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Segese kwenye kilele cha mashindano hayo yenye kauli mbio ya kuimarisha ulinzi shirikishi vijijini, wananchi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kikamilifu na Uchaguzi Mkuu mwakani kwa kuchagua viongozi wenye sifa.

Alisema kila mwananchi anawajibu wa kushiriki kikamilifu katika uch...aguzi huo kwa kujiandikisha kwenye Daftari la Mpigakura au kurekebisha taarifa zake, ili kutopoteza haki yake ya kumchagua kiongozi anayemhitaji. Alisema kutokufanya hivyo inaweza wakaletewa kiongozi wasiyemhitaji, wakawa wanalalamika kila siku mitaani.

Mtendaji wa Kata ya Segese, Patrick Mahona, alisema, mashindano hayo yanazaidi ya miaka 10 tangu yalipoanzishwa, malengo yake ni kuimarisha ulinzi shirikishi vijijini pamoja na upigaji kura.

Diwani wa Kata hiyo, Joseph Manyala, alisema licha ya kuwahimiza wananchi kushiriki katika uchaguzi kikamilifu, vilevile wanawahimiza vijana kuchukua fomu kwa ajili ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

**Imeandaliwa na Daniel Limbe, (Kakonko), Shaban Njia (Msalala)**

# Mganga: Ugonjwa wa kiharusi ni tishio Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Luzila John, amesema ugonjwa wa kiharusi umeendelea kuwa tishio mkoani humo.

Amesema mwezi mmoja watu zaidi ya 20 wenye tatizo hilo hupokelewa na kulazwa hospitalini hapo.

Dk. John alibainisha hayo juzi wakati akitoa elimu kwa watumishi wa afya hospitalini hapo, juu ya kuchukua tahadhari mapema ya kujiunga na ugonjwa huo.

"Februari hadi Juni mwaka huu, tulipata wagonjwa 108 wenye tatizo hilo, hii inaonesha ni kwa namna gani tatizo ni kubwa na linahitaji kuchukuliwa tahadhari kuanzia kwetu sisi na wananchi," alisema Dk. John.

Aidha, alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), watu milioni 15 hupata kiharusi kila mwaka na katika idadi hiyo asilimia 30 hufariki na 30 wanapona wakiwa na kilema, asilimia zilizobaki wanapona na kurudi kwenye hali yao ya kawaida.

Alitaja baadhi ya magonjwa ambayo husababisha tatizo la kiharusi kuwa ni shinikizo la juu la damu, kisukari, moyo, pamoja na kuwa na mtindo mbovu wa maisha.

Hivyo alitoa ushauri kwa wananchi kuacha matumizi holela ya pombe, uvutaji wa sigara, tumbaku, akisema kuwa ni miongoni mwa visababishi vikubwa vya mtu kupatwa na magonjwa hayo.

Pia, aliwasihi watumishi kuwa na utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara, pamoja na kufanya mazoezi ili kuepukana na magonjwa hayo yasiyo ya kuambukiza.

# WMA yasisitiza umakini matumizi ya vipimo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKALA wa Vipimo Nchini (WMA) umesema siyo kila mizani inaruhusiwa kutumika katika sekta za kilimo, uvuvi, biashara na usafirishaji.

Hivyo, imewataka wafanyabiashara kutambua vipimo vilivyo hakikiwa ili kuepukana na mkono wa sheria.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Vipimo Mwandamizi wa WMA, Mkoa wa Mwanza, Lazaro Joram, wakati wa Maonesho ya 19 ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayoendelea jijini Mwanza yakihusisha nchi za EAC.

Joram alisema kwa mujibu wa sheria za vipimo, mazao yote ya shamba yanatakiwa kufungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100, endapo mkulima atafungasha mazao kwa uzito zaidi ya uliotajwa kisheria atakuwa amefungasha lumbesa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema WMA ipo katika maonesho hayo kuwawezesha wadau kutambua majukumu yake, hivyo kuwataka kufika ili wapate elimu na kutambua umuhimu wa kuhakiki na kutumia vipimo sahihi na aina za vipimo vinavyopaswa kutumika katika biashara.

"Tunazo aina nyingi za mizani lakini siyo kila mzani unaruhusiwa kutumika katika biashara au katika sekta ya kilimo, hivyo ukitembelea banda letu tutakupa elimu ya kutambua mizani sahihi iliyohakikiwa pamoja na kutambua alama zinazowekwa katika vipimo vilivyohakikiwa," alisema Joram.

Ofisa Uhusiano wa WMA, Paulus Oluochi, alitoa wito kwa wananchi kutembelea banda lao ili kujifunza kuhusu matumizi sahihi ya vipimo, lakini pia kuwasilisha changamoto mbalimbali kama zipo ili ziweze kupatiwa ufumbuzi.

Akifungua maonesho hayo juzi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, aliwahimiza wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya vipimo kila mara wanapofanya manunuzi na kuuza bidhaa mbalimbali.

Alisema: "Wizi wa kuchezea vipimo ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na hata vitabu vya dini vinakataza wizi wa vipimo kwa hiyo wafanyabiashara wazingatie vipimo sahihi wasiibie wateja wao."




# BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 13, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Ijue miaka 60 ya ubia China - Tanzania, na karata aliyotumia Dk. Samia Beijing

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa si nchini au Afrika pekee, ni hadi kimataifa, gumzo lililotawala ni Mkutano wa Tisa uliofanyikia jijini Beijing, baina ya Afrika na China, Rais Xi Jinping, akiwa mwenyeji wao.

Kikubwa ndani yake, kimetawala yaliyoamuliwa na kutangazwa rasmi na China, uwekezaji wa China Dola za Marekani Bilioni 51, ikiangaza kukopesha nchi za Kiafrika kwa maendeleo hasa ya miundombinu, vilevile haikukaa mbali a na ushirikiano wale wa kihistoria, kwamba iko tayari kutoa msaada wa kijeshi, ikitaja kiwango maalum cha fedha.

China inahitaji nini? Hapo ikaweka wazi kwamba inachotarajia kutoka Afrika ni soko la bidhaa zake. Hivyo kuna 'nipe nikupe,' ikizingatiwa baada ya kuvunja Dola Kuu la Mashariki Duniani (Warsaw Pact) dhidi ya Magharibi, China ikajipanga tena kiuchumi na sasa ni taifa linalotisha kiuwezo katika ulimwengu wa soko, hata kuinyima usingizi Marekani na mshirika wake, nchi za Jumuiya ya Ulaya (EU).

Ni hoja iliyozua mjadala wa kidunia, kwamba uamuzi huo wa China una maana gani, ingawaje hatua kama hiyo ilishachukuliwa na Marekani, pia Russia, kuingia makubaliano ya kibiashara.

Lakini katika namna ya kipekee, Tanzania na jirani yake Zambia zimeonekana kuwa zimetupa karata zao mapema, wakiwa katika hatua ya kutiwa saini makubaliano ya awali ikihusu ukarabati wa reli yao ya TAZARA, ambayo imeharibika na haiko katika ufanisi.



Rais Samia Suluhu Hassan, alipokuwa kwenye mazungumzo na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema katika ofisi za Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU) Addis Ababa nchini Ethiopia, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

Ni reli iliyojengwa kati ya mwaka 1970 na 1975, kwa mkopo usio na riba kutoka China. Hilo linafanya kwa anayehoji kulikoni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Haiakinde Hichilema, wamevuka vipi kuifika hatua hiyo.

Pia, mkuu huyo wa Zambia, naye akatikisa kwa nafasi yake, kwa makubalino kama hayo huko Beijing, kukaundwa mradi wa umeme nchini kwake kwa msada wa China.

**TANZANIA NA CHINA**

Mzizi wa Tanzania na China kuingia uhusiano rasmi ni mwaka 1964, nchini kulipofanyika uamuzi mkuu wenye sura nne; Mosi, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kuunda Tanzania; taifa kuingia katika muundo wa kisiasa na utawala hodi, siasa ya chama kimoja.

Pia, ni mwaka ilipoundwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ikichukua nafasi ya awali iliyoanza nayo kutoka uhuru wa nchi, historia ambayo imeshaelezwa kwa kiasi kikubwa katika maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo yanayoendelea.

Mwisho, ni kuundwa kwa Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Nchi (1964- 1969), ambao hasa ulitafsiri namna nchi inajipanga hasa kwa upande wa Bara na ukaendelezwa kwa miaka iliyofuata.

Ni mpango ambao unabeba sura kamili ya kinachopaswa kufanywa na Tanzania kwa miaka yote tangu wakati huo, ukiwa mfano wa katiba kuu, mipango inaangukia mstari huo hadi sasa.

Katika hatua hiyo ya kwanza mwaka 1964, Tanzania ilikuwa haijajitosheleza kwa mengi na kiuchumi nchini na wananchi wake waliokuwa wasichokizalisha na kuazalisha wasichokitumia.

Mapengo yalikuwa dhahiri katika sekta zote, elimu fursa zake zilikuwa chache na walioelimika na wataalamu walihesabika na mapengo kama hayo katika sekta muhimu kama za kilimo, afya, biashara na viwanda.

Hapo maana yake serikali ya Tanzania ilipaswa kuwezaje kwa kina katika kujitosheleza kufanikisha hilo, huku uwezo wa kiuchumi nchini ulikuwa chini sana, maana ni miaka mitatu tu tangu kupatikana uhuru.

Moja ya mataifa rafiki ambayo hata katika sera za kisiasa ziliendana na nchi ilikuwa China na

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

UBIA WA BENKI DUNIA, TANZANIA, KENYA, ETHIOPIA...

# Mtaji mpya wa maendeleo; uwekezaji darasani, vyuo ufundi, mavuno mara tu baada kuhitimu

• Vituo vya umahiri vyuoni vyaibua umahiri wa teknolojia, hadi uchumi

**Na Grace Mwakalinga**

MARA zote hatua za kimaendeleo ambazo daima huakisiwa katika mustakabali wa uchumi, suala la uwekezaji katika taaluma hupewa msingi mkubwa na kadri unavyokuwa mkubwa, matokeo yanashuhudiwa katika maendeleo ya nchi.

Hiyo inashuhudiwa hata nchini, tangu siku ya kwanza kupatikana uhuru mwaka 1961, hadi sasa, uwezekaji katika elimu kwa ngazi zote, umekuwa na nafasi ya kipekee na endelevu.

Ni hatua inayochukua nafasi kuanzia chini hadi kileleni, kwa maana ngazi ya kujua kusoma na kuandika hadi elimu ya shahada ya falsafa. Hiyo inaendana na shughuli mbalimbali za kitafiti.

Matokeo yake kwa jumla, yamekuwa yakirejewa katika maisha ya kijamii ya kila siku, iwe tiba, biashara, mawasiliano na kila nyanja inayotumiwa na wakazi hao, ikijumuishwa na kinachoendelea duniani.

Katika karne ya 21, Maendeleo ya Teknolojia, Utafiti na Elimu ni nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa mataifa.



Shughuli za ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, ilipoendelea katika tawi lake la Mwanza mwaka jana, ikiwa ni sehemu ya mradi huo wa Benki ya Dunia na serikali. **PICHA: MTANDAO**

### KINACHOJIRI NCHINI

Inaelezwa, kabla ya uwekezaji wa vituo vya umahiri nchini, sekta ya elimu ilikabiliwa na changamoto kubwa, kama inavyooneshwa katika Ripoti ya Kamati ya Bunge ya Elimu ya Mwaka 2018, asilimia 40 ya shule nchini zilikuwa na miundombinu duni.

Hiyo ikaendana na kutokuwapo vifaa vya kisasa, ulioathiri zaidi ya asilimia 60 ya shule na kusababisha kuwapo elimu duni nchini, huku asilimia 25 ya wanafunzi wana matatizo ya kuelewa kwa undani masomo yao kutokana na ukosefu wa vifaa vya kisasa.

Kwenye sekta ya ajira hali ilikuwa mbaya, Ripoti ya Benki ya Dunia (2017), ikibainisha asilimia 70 ya vijana walikabiliwa na changamoto ya ajira za kitaaluma zinazohitaji ujuzi maalum.

Utafiti uliofanywa na Tume ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTEVET) (2020) ulibainisha kwamba asilimia 50 ya wahitimu walikuwa na ujuzi mdogo wa vitendo, ikasababisha ugumu wa kupata ajira. Upungufu huo ulitokana na ukosefu wa mafunzo ya vitendo na uwekezaji mdogo katika sekta za viwanda na teknolojia.

Baada ya muda inatwa hata hivyo, uwekezaji katika vituo vya umahiri nchini, umepata hatua mpya ya maendeleo, kuibuliwa nguzo kama vile Kituo cha Mafunzo ya TEHAMA (RAFIC) cha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT).

Kwingine kunahusu Kituo cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji (CoEATO) cha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Nishati Jadidifu (KIKULETWA) cha Chuo cha Ufundi Arusha.

Aidha, kunatajwa Kituo cha Umahiri cha Uchakataji Ngozi (CELPAT) cha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Mwanza.

Ripoti ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2022 na utafiti uliofanywa na Tume ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTEVET), uwekezaji katika vituo vya umahiri unatarajiwa kuboresha ujuzi wa wahitimu kwa kiasi kikubwa.

Kuna Mradi wa Kujenga Ujuzi na Ushirikiano Afrika Mashariki (EASTRIP) kwa nchi za Tanzania, Ethiopia na Kenya ulioanza mwaka 2019, na ukileta mabadiliko makubwa kupitia uanzishwaji wa vituo vinne vya umahiri nchini.

EASTRIP inatekelezwa na serikali za Kenya, Ethiopia na Tanzania katika vituo 16 vya umahiri kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kuanzia mwaka 2019 na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, ambaye ni Mratibu wa Mradi huo, Fredrick Salukele, anasema vituo hivyo vya umahiri vimejengwa kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda, Afrika Mashariki (EASTRIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Ulianza mwaka 2019 na hadi 2024, ilishagharimu, zaidi ya shilingi bilioni 172.

Akizungumza katika mjadala wa utekelezaji wa mradi huo katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Dar es Salaam, Salukele anasema, malengo ya mradi yanajumuisha kuongeza upatikanaji na uboreshaji programu katika Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Kikanda (TVET).

Anasema, mradi huo umesaidia kutoa elimu bora na ujuzi wa kitaaluma katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), walikojenga Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Nishati Jadidifu, eneo la Kikuletwa wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Anasema ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 90, kukitarajiwa kukuza matumizi ya nishati jadidifu, ikiwamo safi ya kupikia, ambayo kwa sasa inapiganiwa kutumika nchini, kukabili mabadiliko ya tabianchi yanayochangiwa na shughuli za kibinadamu kama kutumia mkaa na kuni.

Salukele anasema, kituo hicho kutapunguza utegemezi wa vyanzo vya nishati nyinginezo, ambazo sio rafiki kwa mazingira na mbadala wake ukitumika.

Anataja nafasi ya Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya TEHAMA (RAFIC) chuoni DIT, Dar es Salaam, kitasaidia kuboresha viwango vya mafunzo katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kwa kutumia mbinu za kisasa, darasani na nje ya darasa.

Anataja maeneo, yanajumuisha wahitimu wenye ujuzi wa wanaoweza kukabiliana na changamoto za kidigitali, pia wakiimarisha uwezo wa vijana nchini, ambao kwa sasa una umuhimu mkubwa katika uchumi wa kidijitali.

"Kupitia mafunzo hayo, vijana watakuwa na ujuzi wa kubuni na kuendeleza teknolojia mpya ambazo zitawasaidia kuanzisha biashara za kiteknolojia, kuzalisha ajira na kuongeza ushindani katika soko la ajira, pia itachangia kuimarisha uchumi wa nchi kwa kuongeza tija na ufanisi katika sekta za teknolojia na mawasiliano," anasema Salukele.

Anaendelea: "Kituo hiki kitachangia kuboresha miundombinu ya teknolojia nchini kwa kutoa wataalamu wenye ujuzi wa kisasa ambao wataweza kuchangia katika miradi mikubwa ya kitaifa na kimataifa, kuimarisha matumizi ya teknolojia na kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi na kijamii," anasema.

Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji (CoEATO), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Salukele anasema, kitasaidia kuimarisha sekta ya usafiri wa anga na ardhi kwa kutoa mafunzo ya kina kwa wahandisi wa ndege, wataalamu wa usafiri wa anga, na maofisa wa usalama wa usafiri.

Anasema kituo hicho kitakuwa msaada wa kuboresha usalama wa anga na ufanisi wa huduma za usafiri, hivyo kuongeza usalama na uaminifu wa miundombinu ya usafiri nchini, vijana watakuwa na ujuzi wa

kupitia mafunzo haya, anaeleza vijana watakuwa na ujuzi wa kitaaluma wa hali ya juu katika sekta ya anga na usafiri, itasaidia kupunguza tatizo la ajira na kuongeza tija katika sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa taifa.

### KUTOKA MWANZA

Akizungumzia Kituo cha Umahiri cha Uchakataji Ngozi (CELPAT) kwa DIT, Kampasi ya Mwanza, Augustine Mbitila, anasema wameanzisha programu zinazoendana na mahitaji ya soko, akidokeza kuwa kati ya mitaala 15 waliokubaliana kuanzisha, kwa sasa wanatumia nane, zote zikionyesha matokeo mazuri, baada ya wanafunzi kumaliza na kupata ajira.

Anasema, kwa hatua zaidi, chuo chake kinafuatilia maendeleo ya kila mwanafunzi mhitimu kujua ujuzi wake na namna ya kumsaidia, apate ajira au kuajiriwa, jukumu ambalo ni la miezi tangu kumaliza masomo.

Salukele anasema, mwaka jana waliwatembelea wahitimu 52 katika maeneo mbalimbali nchini kukagua wanachokifanya, kutokana na ujuzi wa masomoni.

Mwongozo wa mradi huo, ni kila mwaka wanawafikiwa wahitimu 25, lakini anasema wao walivuka lengo ikiwamo namna ya kuwasaidia kukabiliana na soko la ajira.

### KIWANDA CHA CHUO

"Chuo chetu kina viwanda viwili vyenye miundombinu na teknolojia ya kisasa, ambayo hutumika kuchakata ngozi na kuzalisha bidhaa kama vile, mabegi, mipira, majaketi, viatu na mikoba," anasema Mbitila.

Anasema mwanafunzi anashiriki mafunzo kwa vitendo na chuo kimeingia makubaliano na viwanda vinavyotengeneza bidhaa za ngozi, wakivitembelea kujifunza zaidi teknolojia mpya na wanatembelea vingine nje ya nchi, ikiwamo Kenya na Ethiopia.

Anafafanua mikakati hiyo inawasaidia wahitimu kubobea na kuwa wajuzi kwenye sekta za uchakataji ngozi, usindikaji na utengenezaji bidhaa zinazotokana na ngozi kama vile mipira, viatu, mabegi na mikanda.

Mbitila anasema, kuna tija inayoonekana, kwa sababu wanapokea wanafunzi wa kigeni, wanaofika kujifunza teknolojia mpya za kuchataka ngozi na kuongeza tija na ubora wa bidhaa.

"Tunatoa mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za uchakataji na utengenezaji wa bidhaa. Hatua hii imeongeza ushindani kwenye soko la kimataifa ukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo kiwanda cha ngozi mkoani Mwanza kilikufa," anasema Agustine.

Mkuu wa Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji (CoEATO) cha NIT, Dk. Chacha Ryoba, anasema mradi huo umeleta vifaa na mitambo mipya ya kisasa ya kufundishia na kujifunzia, inayochangia kuboresha miundombinu ya usafiri nchini.

Anataja, hatua hiyo inafanikishwa kwa kupatikana wataalamu wenye ujuzi na watakaosaidia katika miradi mikubwa ya miundombinu ya usafiri, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya ndege, miundombinu ya usafiri wa ardhini, majini na reli.

Dk. Ryoba pia anasema, vijana wahitimu wa chuo hicho wameajiriwa katika maeneo tofauti, ikiwamo Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), mashirika binafsi ya ndege na Treni ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR).

Anaongeza kuwa kupitia utafiti na mafunzo, NIT inasaidia kuendeleza teknolojia mpya katika sekta ya nishati, ambayo inaweza kubadilisha sekta hiyo nchini, kutoa fursa za uwekezaji, na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na ubora wa maisha kwa wananchi.

Dk. Ryoba anasisitiza kwamba, kuanzishwa vituo hivyo vya umahiri, kutachochea ukuaji uchumi, kwa sababu kila kituo kinachangia kutatua changamoto za jamii na kuchochea maendeleo ya taifa.

Anaeleza, uboreshaji miundombinu, ikiwamo ujenzi wa madarasa na hosteli kwa ajili ya malazi ya wanafunzi, utaongeza uwezo wa vyuo vya umahiri kupokea wanafunzi zaidi. Anabainisha kwamba mradi ukikamilika, wanatarajia kupokea wanafunzi takriban 2,500, kati yao 2,100 watasoma kozi ndefu na 400 kozi fupi.


Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sylivia Lupembe, anasema miradi hiyo nchini na mataifa ya Ethiopia na Kenya, imeboresha elimu na kuwaongezea ujuzi wanafunzi, kuzalishwa ajira, ongezeko la matumizi ya teknolojia, pia uvumbuzi.

"Tanzania mradi huu umefanikiwa kwa asilimia 100, tumekuwa kinara kuwa na Mfumo wa Uhakiki wa Vigezo vya Elimu unaozingatia muundo ambao unawezesha kutambua na kulinganisha viwango vya elimu, mafunzo na ujuzi kwa kuhakikisha wahitimu wanatimiza viwango vya kitaaluma vinavyotakiwa.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania sasa tumeamua kuua hawa mashujaa wetu!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

KUNA tangazo naliona kwenye runinga, likimwonesha mama na mwanawe mgonjwa wakiwa ndani ya daladala, huku akilalamika wakati dereva haoneshi kujali, lakini abiria wanachachamaa na kumtaka apeleke gari zahanati ya karibu.

Dereva anaona umuhimu, anageuza gari na kumwahisha mama na mwanawe katika zahanati ya karibu, ambako anapata matibabu na mengine yanaendelea. Abiria na dereva wanathamini maisha ya mtoto yule ambaye bado mdogo.

Upande mwingine, nasoma magazetini na kusikia redioni, kuwa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), tena Mjumbe wa Sekretarieti ya chama hicho, Mzee Ally Kibao ameshushwa kwenye basi na watu wasiojulikana na kuondoka naye.

Na si kuondoka naye tu, bali kesho yake anakutwa maeneo amekufa na hatambuliki kutokana na kumwagiwa tindikali usoni na mwili unachukuliwa hadi hospitali ya Mwananyamala, Kinondoni, Dar es Salaam. Damu nzito kuliko maji, ndugu zake Mzee Kibao wanamtambua.

Najiuliza, kama kwenye daladala abiria wamechachamaa mpaka dereva anageuza gari hadi zahanati ya karibu kwa ajili ya matibabu ya mtoto yule, inakuwaje kwa abiria wa basi kubwa kushindwa kupambana na dereva alipeleke kituo cha Polisi cha karibu angalau Kibao angenusurika!

Pia, wale wanaojitambulisha kuwa ni wa chombo cha serikali, wanajiamini vipi kuingia gari lenye watu zaidi ya 50 na kumchomoa

Afande mstaafu, baada ya kulitumikia umma, wanachomoka naye ili kumchomoa roho?

Wanajiamini nini katika basi alilomo askari Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, ambaye hata hatoi ushauri kuhusu kituo cha karibu cha polisi ambako Mzee Kibao angenusurisha maisha yake. Inakuwaje lakini?

Afande Mstaafu Kibao, kapoteza maisha kirahisi kama kuku aliyechomolewa tengani na kuchinjwa, mtu ambaye miaka hiyo ya sabini na baadaye alikuwa mstari wa mbele kutetea nchi yake Tanzania dhidi ya majeshi ya Nduli Iddi Amin Dadah! Askari aliyetetea maisha ya maaluni hawa waliompora roho!

Hivi Watanzania kweli tumefikia hatua hiyo ya sasa kuua askari wetu waliotupambania kutoka uvamizi wa wanajeshi wahuni waliovuka mpaka

na kujitwalia ardhi ya Kagera, kweli? Anauawa askari aliyekwepa risasi za Amin na kutupwa Ununio, kweli?

Hakuna ajuaye kuwa Afande Kibao kauawa kwa sababu za kisiasa, kijamii au kishirikina, hakuna ajuaye kuwa waliomwua kweli ni askari wa vyombo vya dola la Tanzania na hakuna ajuaye watu hao walipata wapi silaha walizo nazo zilizotisha abiria, kondakta na dereva wa basi hilo mchana

kweupe.

Lakini, Watanzania tunajua kabisa kwamba, kuna watu wamepewa dhamana ya kutulinda na mali zetu muda wote na wanalipwa kwa hilo.

Iweje sasa watu wanasimamisha gari la abiria tena si porini, mjini na kumshusha mtu na kuondoka naye bila wasiwasi?

Si hivyo tu, mauaji ya Afande Kibao ni kama yametonesha donda kubwa walilonalo wananchi, kutokana na matukio mengi mengi ya utekaji na mauaji ya Watazania wenzao, hivyo kuhitaji hatua madhubuti za kukabiliana na wimbi hili.

Sawa, Rais ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ametoa tamko, akitaka vyombo vinavyohusika kuchunguza na kuja na majibu. Shida yangu ni namna wanavyochunguza, kama wahusika watatoka humohumo. Nionavyo, kwa nini Tume ya Majaji isitumike hapa?

Lakini, kana kwamba haitoshi, tukumbuke nyuma, mauaji ya mahabusu yalipotokea Shinyanga mwaka 1976, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ali Hassan Mwinyi alijiuzulu kwa kuwajibika kutokana na dhamana yake kwa usalama wa raia na si kwamba alishiriki mauaji, la hasha!

Kama inapendeza, hatua kama kwa nini isichukue nafasi kwa mwenye dhamana, ili kupumzisha akili yake na ya wananchi, kutokana na wimbi hili la utekaji ambalo sasa limeingia mpaka kwenye mauaji ya askari wa akiba, shujaa wetu wa vita vya Kagera?

Ni fedheha kubwa kuona Watanzania wanapotea, wanashambuliwa na kulemazwa, huku wengine wakiuawa na kila mara kutangaziwa wahusika ni watu wasiojulikana. Ina maana, watu hao wako juu ya vyombo vya dola?

Yaani wanaweza kuamua hatima ya maisha ya mtu bila hatua kuchukuliwa kweli? Watanzania itupendeze kusema imetosha na Tanzania tuione ikirejea kuwa kisiwa cha amani, utulivu na upendo kama zamani. Inshallah!

UCHUMI

## YASIYOJULIKANA BANDARI LIULI 1914- 2024...

# Ilivyoanzia mtaji Vita Dunia, hadi historia mkoa, utalii, usafiri ziwani

**Na Gideon Mwakanosya, Nyasa**

BANDARI ndogo ya Liuli mwambao wa Ziwa Nyasa wilayani Nyasa, Mkoa wa Ruvuma, inajulikana hasa kutokana na Hospitali ya Mtakatifu Anna ya Kanisa la Anglikana, inayohudumia wagonjwa wengi katika Wilaya ya Nyasa.

Pia katika usafiri wa majini Ziwa Nyasa, ni bandari muhimu kwa upande mmoja katika usafiri kutoka Bandari ya Itungi, Kyela mkoani Mbeya na mpakani na Malawi kwa upande mwingine, iwe njia ya majini au barabarani.

Katika Sekta ya Utalii, Bandari ya Liuli ni eneo lenye utajiri wa vivutio vya utalii wa aina mbalimbali. Jina Liuli lina maana ya 'jiwe lile'.

Wakati wa ukoloni wa Kijerumani Liuli iliitwa "SPHINXHAFEN" yaani bandari ya SFINKSI kwa sababu ya kuwapo utajiri wa miamba mikubwa inayofanana na sanamu mashuhuri kwenye 'Piramidi za giza kama nchini Misri.'

Mnamo Agosti 13, mwaka 1914 mwanzoni mwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Waingereza walishambulia katika eneo la Liuli meli ya pekee ya Wajerumani kwenye Ziwa Nyasa, ambako katika jiwe kubwa la Pomonda lililoko mita 300 ndani ya Ziwa Nyasa, ikitumika kuwa maficho ya askari wakati wa vita.

Kwa mujibu wa habari katika gazeti la Times iliyochapishwa mwaka 1914, Uingereza iliwahi kuingia katika vita ya kwanza ya dunia Agosti 4, 1914 na kwamba siku chache baadaye Nahodha Mwingereza Edmund Rhoades katika kisiwa cha Nkhata Bay nchini Malawi.

Alipokea amri ya kuzamisha meli Hermann von Wissmann iliyokuwa meli pekee ya Wajerumani kwenye Ziwa Nyasa.



Jiwe la kihistoria lililoko katika Bandari ya Liuli Ziwa Nyasa mkoani Ruvuma, lililotumika kama maficho katika Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia 1914 hadi 1918. **PICHA ZOTE: GIDEON MWEAKANOSYA**

Meli hii ilikuwa chini ya Nahodha wa Kijerumani aliyeitwa Berndt, ambayo baada ya kupata amri, Rhoades aliendesha meli yake HMS Gwendolyn kuelekea Sphinxhafen (Liuli), kwa sababu alijua meli ilikuwa wapi.

Manahodha wote wawili walikuwa marafiki waliowahi kutembeleana mara kwa mara na kukaa pamoja.

HMS Gwendolyn ilipokaribia Bandari ya Liuli, mpigaji mizinga wa pekee wa meli na mfanyabiashara mmoja Mskoti alikuwa mtu wa pekee mwenye kujua matumizi ya mzinga, hivyo alianza kufyatua risasi dhidi ya Hermann von Wissmann.

Dakika chache baadaye, boti ndogo ilikaribia haraka HMS Gwendolyn. Nahodha Berndt akapanda meli na kumwuliza mwenzake kwa hasira, kwa nini amelewa wakati wa mchana.

Hakujua kuwa vita ilianza tayari katika bara la Ulaya hivyo, Rhoades alimtangaza nahodha wa Kijerumani kuwa mfungwa wa vita.

Habari ya ushindi huo ilipelekwa London kwa simu na Agosti 16, mwaka 1914, gazeti la Times lilichapisha na kutangaza ushindi wa Uingereza katika Bandari ya Liuli Ziwa Nyasa "Naval Victory on Lake Nyasa".

Wakati huo, Waingereza waliondoa mzinga mdogo wa meli na vipuli kadhaa ili meli isitumike tena bila kuiharibu. Mwaka 1915 Wajerumani walikuwa wameleta tena vipuli na kutengeneza meli ambapo Waingereza walirudi Liuli na kuzamisha meli ya Hermann von Wissmann katika Bandari ya Liuli.

Baada ya vita, meli ilifufuliwa tena na kufanya kazi kwa Waingereza ambayo hadi sasa maboya yamewekwa katika eneo la Liuli, kuonesha mahali meli hiyo ilipozamishwa.



Meli ya Wajerumani iliyozamishwa na Waingereza mwaka 1914, katika Bandari ya Liuli, Ziwa Nyasa, mkoani Ruvuma.

## IJUE MIAKA 60 YA UBIA CHINA - TANZANIA, NA KARATA ALIYOTUMIA DK. SAMIA BEIJING

Inatoka Uk 11

kwa maana hiyo, Rais Mao Tse Tung na Mwalimu Julius Nyerere, wakaanza kufanyia kazi.

Moja ya mazao yake ya awali katika hilo, ni kutoa usaidizi kwa staili ya kujengea uwezo nchi, ikiwamo katika sekta kama Ulinzi na Usalama na ikizingatiwa katika upande wa pili wa shilingi, hali za ukoloni mamboleo na mapinduzi Afrika, yalikuwa juu sana wakati huo, nchi nyingi zikitoka kupata uhuru.

Mwaka 1967, serikali ikiwa inatekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo na kukafanyika Azimio la Arusha, iliyoweka miradi yote kitaifa katika himaya ya serikali. Mwaka mmoja baadaye, kupitia mazungumzo binafsi ya marais Mao Tse Tung, Kenneth Kaunda na Mwalimu Nyerere, upakatikana mradi wa TAZARA.

Nyerere na Kaunda wakiwa waumini wa itikadi moja, chini ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika, wakaingia katika mradi huo wa TAZARA mwaka 1970 ambao ni wa kiuchumi, pia upande wa pili siasa, ukikwepa matumizi ya bandari za Msumbiji kuliokuwa koloni la Ureno, pia utawala wa makaburu wa Afrika Kusini.

Miaka yote baada ya hapo, China imedumu kuiwa mshirika wa Tanzania, ikijidhhirisha katika matendo ya kihistoria, kundi kubwa la Watazanania hadi miaka ya 1980 wakarejea kutoka USSR na China na madakatari wengi wa Hospitali ya Ocean Road na Muhimbili, Dar es Salama wakiwa wahitikimu wa nchini hizo, huku USSR ikiwa na chuo kikuu malaum kwa Waafrika Lumumba.

Kwa maana hiyo, ndani ya uhusiano wa kudumu wa Tanzania na China, mradi mpya wa Hichlime na Dk. Samia, wametumia kuwa karata yao ya maendeleo, hata kupatikana mradi huo wa TAZARA, wakijinadi nao mapema hata kabla ya mkutano wa Bejing wiki iliyopita. Katika sura nyingine imekuwa mradi wake maalaum Rais Dk. Samia katika mikakati mipyo yake kimaendeleo ambayo nchi inayo katika uhusiano na China.

Sura nyingine ya uhusiano katika siasa, inajionyesha hata katika ziara mahsusi ya Rais Xi Jinping, wastani wa miaka tisa iliyopita, akiwa na kundi kubwa la wafanyabiashara waliofika.

Pia, katika ziara za awali ugenini, Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo, katika ziara za awali akaifanya nchini China, kama alivyofanya Rais Samia, ikiashiria uwekezaji wake huko. Majumuisho ya yote inaanika ishara ya ubia wa Tanzania, Zambia kwa Wachina.



# Tanzania ya 25 duniani matumizi ya TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imetajwa kuwa moja ya nchi 25 bora duniani kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye kutoa huduma za serikali.

Mkurugenzi wa Tume ya TEHAMA nchini (ICTC), Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kongamano la TEHAMA ambalo hufanyika Oktoba kila mwaka. Alisema Tanzania kuna huduma nyingi zinapatikana kwa njia ya mtandao ikiwamo kulipia ankara hata mtu akiwa nje ya nchi.

"Ukiangalia vipimo mbalimbali kuhusiana na mambo ya TEHAMA duniani sisi tunafanya vizuri tunapaswa kuacha kujidharau, huko duniani tunaheshimika kwa mfano katika kutoa huduma za serikali ni kati ya nchi 25 bora duniani kwa uwezo huo," alisema.

Alisema kutokana na sifa hiyo, Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa kongamano kubwa la kimataifa la akili mnemba.

"Hizo huduma haziwezi kufanya vizuri kama huduma za mtandao hazipo vizuri. Kuna vitu vingine vingi wakitupima sisi tunakwenda vizuri, sasa kutokana na hilo kuna haya mashindano ya Afrika ya vijana ya akili mnemba na mambo ya roboti kwa mara ya kwanza Afrika yanafanyika hapa nchini," alisema.

**"Hizo huduma haziwezi kufanya vizuri kama huduma za mtandao hazipo vizuri. Kuna vitu vingine vingi wakitupima sisi tunakwenda vizuri, sasa kutokana na hilo kuna...**

Aidha, alisema kupelekwa kwa roboti Eunice bungeni kuliipa Tanzania heshima nje ya nchi ya kuwa na uwezo wa kujiamini wa kupeleka teknolojia hiyo bungeni.

"Unajua kuna aina 16 za roboti, unajua watu wengi wameanza kumjua roboti kupitia kwenye sinema nadhani hiyo ndiyo inawachanganya wengi, roboti ni akili mnemba ambayo kompyuta ipo ndani, huku nje mwonekano wake ni mdoli tu, kama Eunice alivyokuwa akisalimia kilichokuwa kinafanya atoe mkono ni komputa iliyokuwa ndani yake ni software," alisema.

Alisema kwenye kongamano hilo litakalofanyika Oktoba 13-17, mwaka huu watakuja watu wa nchi mbalimbali kutoka Afrika kushiriki mashindano hayo ya kwanza.

Alisema: "Tumejipanga sisi kama nchi kuna vijana wengi wamejitokeza kwenye haya mashindano kwa hiyo watatangazwa pale katika kongamano, pia tumetoa nafasi kwa vijana kuja kuonesha uwezo wao kwa siku tano."



Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary (wa tatu kulia), akisoma majina ya wateule wa Mufti wa ngazi mbalimbali za uongozi wa baraza hilo, wakati wa kikao kilichowahusisha masheikh, maimamu, walimu, idara ya vijana na wanawake, katika Msikiti Mkuu wa Gadafi, jijini Dodoma juzi. Wengine kutoka kulia ni Katibu wa BAKWATA wa wilaya hiyo, Ustaadh Ahmed Msuri, Kaimu Sheikh wa wilaya hiyo, Abdallah Msafiri na baadhi ya wadau wa baraza hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Korea Kusini yapiga 'tafu' vifaa sekta ya afya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kimataifa la Maendeleo la Korea Kusini (KOICA), limetoa vifaa kwa ajili ya kufunga Mfumo wa Serikali wa Kusimamia Huduma za Afya (GoTHOMIS), ambao utasaidia kuimarisha huduma katika vituo vya afya Mkoa wa Dodoma.

Vifaa hivyo vina thamani ya Dola za Marekani milioni 6.2 kwa ajili ya mfumo huo wa kuangalia taarifa pamoja na kumbukumbu za matibabu ya mgonjwa ikiwamo utoaji dawa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa hafla ya makabidhiano ya vifaa hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2021 na leo (Jana), wamepokea vifaa hivyo.

Hivyo, aliishukuru KOICA kwa msaada huo wa vifaa vilivyotokana na ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea.

Alifafanua kuwa vifaa hivyo vitakwenda kufungwa katika hospitali za wilaya nane, vituo vya afya 55 pamoja na zahanati 172 mkoani Dodoma.

"Kufungwa kwa mfumo huu unakwenda kupunguza adha ya utafutaji faili la mgonjwa kwa ajili ya kuona taarifa za matibabu za awali, naishukuru sana serikali kwa kuweka uhusiano huu mzuri baina ya Korea, wamekuwa wakiunga mkono sekta ya afya kwa miaka mingi hapa nchini na hii inatokana na ushirikiano mzuri baina ya nchi hizi mbili,"alisema Senyamule.

Hivyo, aliwaagiza wakurugenzi wa wilaya kuhakikisha wanavifunga mara moja vifaa hivyo ili mfumo huo uanze kutumika.

Mkurugenzi Mkazi wa KOICA, Manshik Shin, alisema wametoa vifaa hivyo ili kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa nchini hususani mkoani Dodoma.

Alisema vifaa hivyo vitatoa urahisi kwa wahudumu wa afya, pamoja na ufanisi katika utoaji huduma kwa wagonjwa pale daktari anapohitaji kupata taarifa za nyuma ili ampatie tiba sahihi mgonjwa.

Naibu Katibu Mkuu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Grace Magembe, aliwashukuru KOICA, huku akisisitiza wataendelea kushirikiana ili kuendelea kuimarisha utoaji huduma za afya.

# TAWA: Wananchi anzisheni mashamba ya wanyamapori

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa kwa kuanzisha mashamba ya wanyamapori katika mikoa yao yenye hifadhi, ili wajipatie kipato na kujikwamua na umaskini.

Ofisa Mhifadhi Wanyamapori Kanda ya Kati, Ogossy Gasaya, alitoa rai hiyo jana kwenye Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Mifuko ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yanayofanyika kitaifa mjini Singida. Alisema wamekuja kutoa elimu kwasababu wananchi wengi bado hawajui kama kuna fursa za kiuchumi zilizoko Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia TAWA.

Gasaya alisema miongoni mwa fursa zinazopatikana ni pamoja na uanzishaji wa mashamba ya ufugaji wanyamapori, mabucha ya kuuza nyamapori.

Alisema katika fursa ya uanzishaji mashamba ya wanyamapori yaliyopo na mikoa yao wananchi wanaweza kutengeneza ratiba maalum ya kutembelea maeneo hayo na hivyo kujipatia pesa.

"Wananchi wakichangamkia fursa ya kuanzisha mashamba ya wanyamapori, TAWA inatoa mbegu na mwongozo wa namna ya kuyaanzisha hayo mashamba ambapo miongozo yote inapatikana katika ofisi za TAWA zilizopo kwenye kanda zote," alisema. Gasaya alisema kwa upande wa uhifadhi, TAWA haipendi kuona wananchi wanalipiza kisasi kwa kuwaua wanyamapori wanapoharibu mazao yao, hivyo imekuwa ikitoa elimu ili waendelee kuwa rafiki wa wanyamapori na kutoa taarifa kwa mamlaka zinazohusika kunapotokea uharibifu umefanywa na wanyama.

Aliongeza kuwa TAWA imekuwa ikitoa Dola za Marekani 5,000 kila mwaka zinazotokana na uwindaji wa kitalii kwa vijiji vinavyopakana na hifadhi, ili waendelee kuona umuhimu wa uhifadhi na kutoa ushirikiano.

Alisema pia asilimia 25 ya makusanyo ya jumla ya shughuli za utalii inayotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa vijiji vinavyopakana na mapori ya uhifadhi ambayo inatolewa kwa misimu miwili.

Ofisa Wanyamapori Msaidizi Kanda ya Kati, Kanunga Marau, alisema TAWA kwa kutambua umuhimu wa uchumi wa wananchi imekuwa ikitoa elimu kuhusu wanyamapori waharibifu na wakali.





# Malori yenye taka hatarishi yashikiliwa Kasumulu

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MALORI zaidi ya 46 yenye shehena ya taka hatarishi yaliyokuwa yanasafirishwa kutoka Malawi yamezuiwa kwa zaidi ya mwezi mmoja katika mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela, kutokana na kukosa nyaraka za usafirishaji wa taka hizo.

Baadhi ya taka ngumu zilizobebwa kwenye malori hayo ni pamoja na vyuma chakavu ambavyo inadaiwa kuwa zinasafirishwa kwenda nje ya nchi.

Juzi, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, ilifanya ziara katika eneo yalipoegeshwa malori hayo na kuzungumza na madereva ambapo waliiomba serikali kuwaruhusu kuondoa magari yao katika eneo hilo kwa maelezo kuwa wamekwama kwa muda mrefu.

Mmoja wa madereva hao, Abubakar Said alisema pamoja na kukaa muda mrefu katika eneo hilo bado hawajaambiwa kosa lao ni nini, hali ambayo inawafanya washindwe kuelewa.

Alisema kwenye maelezo waliyopewa ni kwamba kwenye malori hayo wanaweza wakawa wamebeba mabomu jambo ambalo siyo kweli kwa maelezo kuwa wangekuwa wamebeba vitu hivyo vingekuwa vimeshaleta madhara.

"Kama ni mabomu mpaka sasa yangekuwa yameshalipuka na kusababisha madhara, sasa tunashindwa kuelewa ni nani mwenye kosa kati yetu sisi madereva na mamlaka ambazo zinadhibiti taka hizi?" alihoji Abubakar.

Naye Abdallah Mohamed alisema magari yao yalizuiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambalo halina wawakilishi kwenye mpaka huo na hivyo wanashindwa kupata elimu sahihi ya usafirishaji wa taka hizo.

Hivyo, aliiomba serikali kudhibiti taka hizo kabla hazijaingia nchini badala ya kuanza kuzuia zikiwa tayari zimeingia nchini na kuanza kuweka vikwazo ambavyo vinawaumiza Watanzania.

**"Kama ni mabomu mpaka sasa yangekuwa yameshalipuka na kusababisha madhara, sasa tunashindwa kuelewa ni nani mwenye kosa kati yetu sisi madereva na mamlaka ambazo..."**

"Hizi taka kama ni hatarishi basi serikali ingeweka utaratibu wa kuzizuia zisivuke mpakani, kitendo hiki cha kuruhusu ziingie kwanza zikaleta madhara kwa wananchi," alisema Abdallah.

Mwakilishi wa NEMC Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini, Johanes Karungura ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria alisema Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inaelekeza kwamba mtu yeyote anayesababisha uchafuzi wa mazingira kwenye nchi nyingine anatakiwa kulipia uchafuzi huo.

Vilevile, alisema kitendo cha kusafirisha taka hatarishi kutoka nchi moja kwenda nyingine bila mamlaka za udhibiti wa taka hizo za pande mbili kuwasiliana ni kosa kisheria na inatakiwa hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema baada ya malori hayo kushikiliwa katika mpaka huo, ilitolewa amri kutoka NEMC makao makuu kwamba sheria ifuatwe kwa kuhakikisha wasafirishaji wa taka hizo wanalipa faini ambayo haikutajwa bayana.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema maelekezo ya NEMC ilikuwa ni kila lori linatakiwa kulipiwa Sh. 6,000,000 ambapo kwa idadi ya malori yaliyopo wenye malori walitakiwa kulipa zaidi ya Sh. milioni 270.

Alisema maelekezo yaliyotolewa na serikali ni kwamba faini hizo hazitakiwi kulipwa na badala yake Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ifanye utaratibu wa kupeleka mashine ya kukagua mizigo hiyo ili kubaini kilichobebwa na sheria zifuatwe.

Alisema kitendo cha kutaka faini hizo zilipwe kingewaumiza wenye malori hayo na hivyo akawataka maofisa wa NEMC kuzingatia maelekezo hayo na kwamba yametolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.



Baadhi ya malori yenye shehena ya taka ngumu yaliyozuiliwa katika mpaka wa Kasumulu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya wakati yakitokea nchi ya Malawi kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa, kwa sababu ya kukosa nyaraka muhimu, yakiwa yamezungushiwa utepe, wakati wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo, ilipofanya ziara eneo hilo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakazi Njombe wakoshwa ujenzi kituo cha afya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa Kata ya Kifanya Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, wameishukuru serikali kwa kuwajengea kituo cha afya na kusema kitawasaidia kuondokana na tatizo la kutembea umbali wa kilometa 50 kufuta huduma za afya katika Hospitali ya Kibena.

Walitoa pongezi hizo juzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyofanya ziara ya kutembelea miradi ya Kituo cha Afya Muungano na jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Kibena yenye thamani ya Sh. milioni 773 katika Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Walisema miaka ya nyuma walikuwa wakisafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya jambo ambalo hivi sasa halipo kwa sababu wanatibiwa katika kituo hicho. "Tulikuwa tukisafiri kwenda Hospitali ya Kibena au Ikonda aliyopo wilayani Makete ambako ni mbali tunaishukuru sana serikali kwa kuboresha huduma ikiwamo majengo mapya," alisema Tweve.

Naye Diwani wa Kata ya Kifanya, Nolasco Mtewele, alisema mradi wa Kituo cha Afya Muungano uliibuliwa na wananchi na baadaye serikali ilileta fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya. "Tunaomba mtufikishie salamu zetu kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea fedha na vifaa tiba kwa ajili ya kituo chetu hiki," alisema Mtewele.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Justine Nyamoga aliipongeza serikali kwa kuendelea kusawazisha huduma katika maeneo ya mijini na vijiji.

"Bunge tunaridhishwa sana jinsi miradi inavyotekelezwa popote pale tunapopita na hapa Kifanya ni kielelezo cha uboreshaji cha huduma za afya kwenye maeneo ya nje ya miji, tumeingia chumba cha upasuaji kinafanana kabisa na vyumba vya upasuaji vya kisasa vilivyoko katika maeneo mengine," alisema Nyamoga.

Aidha, kamati hiyo ikiwa katika Hospitali ya Kibena walipotembelea wodi ya watoto waliozaliwa kabla ya kufikisha miezi tisa (njiti), mjumbe wa kamati hiyo, Salome Makamba alishauri kuwekwa runinga katika wodi hiyo ili kuangalia vipindi mbalimbali ambavyo vitawasaidia kinamama hao kuepukana na tatizo la magonjwa ya akili kutokana na kukaa peke yao muda mrefu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali kupitia mapato ya ndani ikiwamo ya sekta afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa ukaribu.

# Viuatilifu vyatajwa kusababisha magonjwa Nyanda za Juu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MATUMIZI yasiyo sahihi ya viuatilifu yametajwa kuwa chanzo cha ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa wananchi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Kutokana na hali hiyo serikali imeiagiza Mamlaka ya Afya ya Mimea na Udhibiti wa Viuatilifu nchini (TPHPA) kuanza kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima na maofisa mbalimbali wa serikali ili kunusuru jamii.

Mafunzo hayo yalianza kufanyika jijini Mbeya kwa siku tano yakiwahusisha wakulima, maofisa ugani na wafanyabiashara wa viuatilifu ili kuhakikisha elimu hiyo inasambaa katika maeneo yote.

Akifunga mafunzo hayo juzi, Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema viuatilifu hivyo vina viambata vya sumu ambavyo ni hatari kwa afya za wananchi na hivyo akawataka maofisa hao kutoa elimu kwa kina.

Alisema kemikali hizo ndizo zimekuwa chanzo cha magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza ikiwamo saratani na hivyo akasisitiza kuongezeka kwa umakini wakati wa kutumia.

"Kwa siku za karibuni magonjwa haya yameongezeka sana kutokana na matumizi holela ya viuatilifu, ninyi wataalamu ndiyo mnaotakiwa kuhakikisha elimu hii inawafikia wakulima wetu, nawapongeza kwa kuanza kutoa elimu hii na naomba mwendelee," alisema Madito.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanashiriki kupeleka elimu hiyo kwa wenzao ili wazingatie matumizi sahihi na kuepuka madhara ya viuatilifu hivyo.

Mratibu wa mafunzo kutoka TPHPA, Jumanne Msalama, alisema ili kukabiliana na madhara ya viuatilifu hivyo wanahakikisha kila aina ya kiuatilifu kinachoingia nchini kinasajiliwa.

Alisema viuatilifu hivyo ni lazima viandikwe kwa lugha ambayo inaeleweka vizuri kwa watumiaji wakiwamo wakulima wa kawaida.



# Dk. Mwinyi: Viashiria vya awali Zanzibar ina madini zaidi ya 11

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema viashiria vya awali vimeonesha kuwapo kwa madini mengi visiwani Zanzibar.

Madini hayo ni yale yanayotumika katika uzalishaji wa saruji, vioo, vigae vya sakafu, saa, bodi za ndege, injini za magari, vifaa vya kuprintia, vioo vya televisheni, baruti, lenzi za miwani, viungo vya bandia na nyenginezo.

Alisema hayo jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa Ripoti ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Zanzibar iliyofanyia visiwani hapa.

Dk. Mwinyi alisema tafiti zaidi zinahitajika katika maeneo husika, ili kumwezesha mwekezaji kufanya maamuzi sahihi ya kuwekeza katika sekta ya madini visiwani humo.

Aidha, alisema mbali na madini hayo, utafiti uliofanyika umegundua maeneo mbalimbali ya kijiolojia ambayo mipango yake yanaweza kuboreshwa na kutumika kama sehemu za vivutio vya utalii, sambamba na dhamira ya serikali ya kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo kikubwa cha utalii.

Dk. Mwinyi alisema: "Lengo ni kuweka mikakati ya kuanzishwa kwa soko la madini katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na idadi kubwa ya watalii tunaowapokea hapa nchini. Kadhalika sekta ya mafuta na gesi nayo itanufaika na utafiti huu pamoja na sekta nyingine kama nilivyozitaja".

Alisema kwa kipindi kirefu kumetokea maafa makubwa katika maeneo mbalimbali nchini hasa nyakati za mvua ikiwamo mafuriko.

Alisema hayo yote yamegusiwa katika ripoti hiyo na kubainisha maeneo husika pamoja na kutengenezewa ramani ambayo itarahisisha kujua maeneo yanayohusika.

Hivyo, aliwataka makandarasi wa majengo na Kamisheni ya Maafa ni vyema kuitumia ripoti hiyo wanapopanga mipango yao ili kunusuru majanga yasitokee.

**Alisema manufaa ya utafiti huo kwa Zanzibar yana maana kubwa na uchumi wa Zanzibar utabadilika, Kisiwa cha Pemba kuna madini mazito ambayo yana mahitaji makubwa...**

Naye Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara, alisema, utafiti uliofanyika ni wa awali na duniaimeifanya Tanzania kuwa mwenyekiti wa udhibiti wa maliasili za baharini, hivyo lazima kujipanga kimaendeleo kutokana na uchumi.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema kazi kubwa inayofanywa na Dk. Mwinyi imeiweka Zanzibar katika ramani ya kati ya nchi zinazofanya vizuri katika ukuaji wa uchumi kupitia uchumi wa bluu.

Alisema manufaa ya utafiti huo kwa Zanzibar yana maana kubwa na uchumi wa Zanzibar utabadilika, Kisiwa cha Pemba kuna madini mazito ambayo yana mahitaji makubwa duniani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini wa SMZ, Joseph Kilangi, alisema ripoti hiyo imebeba mambo mengi muhimu kwa mustakabali wa rasilimali ya nchi.

Alisema pia inahusisha utambuzi wa aina ya miamba, viashiria vya madini na maeneo ya mapango ya asili yanaweza kutumika kama vivutio vya utalii na uwepo wa maeneo yenye uwezekano wa uwepo wa majanga ya asili.

Alisema tangu mwaka 1964 madini yaliyokuwa yakitambulika Zanzibar ni ya ujenzi pekee, lakini kwa mara ya kwanza serikali imefanya utafiti huo ambao umetoa dira na dalili ya kuwepo kwa madini mbalimbali na kuleta mwelekeo mpya.

Alisema utafiti huo ulianza Novemba 2023 na umekamilika Machi mwaka huu na sampuli 169 zilichukuliwa na kupelekwa katika maabara kwa ajili ya uchunguzi na kuainisha madini mengi yalipo Zanzibar.

Mkurugenzi wa Idara ya Nishati na Madini, Said Haji Mdungi, alisema miongoni mwa madini yaliogundulika ni madini ya chokaa.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, akishiriki ujenzi, wakati alipokuwa akikagua mradi wa flemu ya duka katika maskani ya CCM Bwegeza, Jimbo la Kiwani Pemba, juzi. **PICHA: ISIHAKA OMAR**

# Visiwa vidogo Unguja, Pemba hatarini kutoweka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema visiwa vidogo vilivyoko Unguja na Pemba vinakabiliwa na athari kubwa za mabadiliko ya tabia ya nchi, ikiwamo tishio la kutoweka kunakosababishwa na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Mkuya alivitaja visiwa hivyo vidogo ambavyo vinakabiliwa na athari za kimazingira ni pamoja na Kisiwa Panza, Mnemba, Uzi, Kojani pamoja na Makoongwe na Matumbini viliopo Pemba.

Alisema visiwa hivyo vimekumbwa na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na kusababisha tishio kwa wakazi wake kuvihama visiwa hivyo.

Alisema serikali inazifahamu changamoto hizo na imeanza kuchukuwa hatua mbalimbali ikiwamo kujenga kuta sehemu ya pembezoni mwa bahari ili kuzuwia athari hizo.

Aidha, alisema baadhi ya maeneo yameonekana ni bora kujenga kuta ambazo zitazuia kasi ya maji ya bahari kuja juu na kutishia kuingia katika maeneo ya makazi ya wananchi.

Alizitaja juhudi nyingine ikiwamo kuotesha miti ya aina mbalimbali ikiwamo mikoko na mikaa ambayo ni maarufu kwa kuzuia kasi ya maji ya bahari kuingia katika maeneo ya makazi.

# Waziri awatangazia neema wasanii Zanzibar

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, amesema watasimamia kazi za wasanii kwa ubunifu kibiashara, ili wapate kipato na kunufaika kibiashara.

Alisema hayo alipokuwa katika hafla ya ugawaji wa mirabaha katika kutengamana na wadau wa hakimiliki, hafla ambayo ilifanyika visiwani humo.

Alisema haiwezekani wasanii kuburudisha, kuelimisha lakini maisha yao ni duni, hivyo ni vyema waishi kibiashara na kuwa na usimamizi mzuri.

Hivyo, aliwataka mameneja wa Zanzibar wanaowasimamia wasanii kufungua fursa za kibiashara kwa wasanii badala ya kuwa na mameneja wajanja.

Alisema licha ya kuwa kazi ya sanaa ni kuburudisha, kuelimisha na kukosoa jamii lakini ni vyema kwa wasanii kubadilisha mtazamo na kuifanya sanaa kuwa zao la biashara.

"Serikali ipo tayari kuifanya sanaa kuwa ni sehemu ya biashara ili kuwawezesha wasanii kunufaika na kazi zao kupitia nyanja mbalimbali," alisema.

Alisema kuwa haipendezi kuona msanii anafanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi kimuziki na mambo mengine, lakini kipato chake hakiendani na kazi anayoifanya.

Hivyo alitumia fursa hiyo kuitaka Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (COSOZA) kuongeza wigo wa kukusanya mrabaha wa kazi hizo katika maeneo ya kiteknolojia, kwasababu katika maeneo hayo kuna matumizi makubwa ya kazi hizo.

Aidha aliitaka COSOZA kuliwezesha kundi hilo kuuza kazi zao kidijitali ili kwenda sambamba na wakati uliopo, hivyo lazima wasanii kujituma na kuwa wabunifu katika kazi zao hizo.

Ofisa na Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (COSOZA), Mtumwa Khatib Ameir, alisema wasanii na wabunifu wa Zanzibar wakipokea mrabaha inayotokana na matumizi ya kazi zao kibiashara kwa miaka 11 sasa mfululizo.

Alisema kwa mwaka huu Sh. 157,566,640 zimekusanywa kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024, ambapo fedha hizo zimegaiwa katika mgawo huo.

Alisema makusanyo hayo ni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya makusanyo ya Sh. 150,000,000 kwa mwaka wa mgawo wa mwaka 2023/2024.

Alisema katika mgawo huo kiwango cha juu cha mrabaha ni Sh. 3,174,985 na kiwango cha chini ni Sh. 25,000.

Alisema makusanyo ya wafanyabiashara wa sanaa yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka ingawa kiwango cha ongezeko hilo hakiridhishi kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa wasanii kutojisajili.

Alisema kuna wasanii wengi lakini bado kuna mwamko mdogo wa kwenda kujisajili ili kupata usimamizi imara wa kazi zao.

Balozi wa Hakimiliki Afrika, Salum Maulid Salum, alisema licha ya wasanii wengi duniani kuwa matajiri lakini kwa upande wa Zanzibar wengi wao ni maskini.

Alisema katika kufikia malengo ya watu hao lazima serikali kushirikiana na wadau wa sanaa kuja na mikakati itakayosaidia kundi hilo kunyanyuka kiuchumi na kutambulika kama wasanii wa nchi nyengine.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara, Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, Mtumwa Peya Yussuf alisema vijana wengi wasanii wanatumia ubunifu na rasilimali nyingi kutayarisha kazi hizo lakini kipato chao kidogo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JUDITH JEREMIAH KARANGI** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 034278.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/196870/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABSALOMU MORIS ADREA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S1635-0042** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GWANUMPU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. cheti hiki kilipotea Dar es Salaam. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/195937/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FAIGA MAHSEIN TAMIM** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria namba **TAE465641** iliyotolewa uhamiaji makao makuu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/187065/204**

## VIWANJA VINAUZWA

1. KIWANJA **SQM1698** CHA KUJENGA HOTEL KINAUZWA MEDELI WEST, DODOMA MJINI JIRANI MORENA HOTEL NYUMA YA SHOPPERZ BEI TSH 185, 000,000.KINA HATI MILIKI
2. KIWANJA KIKUBWA SQM 4762 KINAUZWA KISASA DODOMA JIRANI NA BARABARA YA MOROGORO BEI TSH MIL 150,000,000

**CALL 0655660730: Instagram@dodoma_deals.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABAN ALLY MSANGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 691 BMR – TOYOTA CARINA**. Chassis namba AT2116062433. Engine namba **A779301** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/33930/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA UBUNGO LILILOKO – LUGURUNI**

**MAOMBI MAKUBWA NAMBA 140 YA MWAKA**

**IRENE CLEOPA MWANRY.............MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**DICKSON SHIO.............MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**DICKSON SHIO...............POPOTE ULIPO**

**IRENE CLEOPA MWANRY** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo lililopo Luguruni/Kibamba. Maombi yamepangwa kutajwa tarehe 15/10/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au Wakili wako kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa.
Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ubungo. Endapo hamtatekeleza/hautatekeleza maombi haya yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) UBUNGO
DAR ES SALAAM

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1440/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAFIDH KHALFAN HUSSEIN WA DAR ES SALAAM**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ADNAD HAFIDH KHALFAN**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 mwezi 10 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 12 mwezi 09 mwaka 2024.

HAKIMU

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DODOMA SUB REGISTRY)**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 17303 OF 2024**

**In the matter of the estate of the late EMMANUEL MAGIBO MURUGA of Dodoma City**
**BY**
**JUMANNE JOHN MURUGA.............................................1ST PETITIONER**
**ZEGERA YOHANA ZEGERA..................2ND PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULE GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 9th day of October 2024 at 09:00 hours
Dated at Dodoma this 10th day of September ......2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DODOMA SUB REGISTRY)**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO. 17584 OF 2024**

**In the matter of the estate of the late EMMANUEL MAGIBO MURUGA**

**AND**

**In the matter of Application for appointment of administrator pendente lite by JUMANNE JOHN MURUGA and ZEGERA YOHANA ZEGERA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULE GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 9th day of October 2024 at 09:00 hours
Dated at Dodoma this 10th day of September 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 279 LA 2024**

**NURDIN SALIM KILUA............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **VICTORIA FINANCE PLC**
2. **YONO AUCTION MART & CO. LTD.....MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **VICTORIA FINANCE PLC**
2. **YONO AUCTION MART & CO. LTD.........POPOTE ULIPO/MLIPO**

**NURDIN SALIM KILUA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 24/09/2024 saa 3:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 04 Mwezi 09, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

## TANGAZO LA MNADA

Held, Rapitech,Kasaroba,Marmboto,Arm auctioneer and Dar state Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Jijini Dar es salaam, Dodoma na Arusha Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Jina la mteja | Aina ya gari | Mahali | Dalali | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fredrick Raphael Mazengo | Toyota OPA T180BZK | Dodoma | Held | 28.09.2024 |
| 2 | Modestar Simon Livigha | Toyota Rav 4 T233DCK | Dar es alaam | Rapitech | 28.09.2024 |
| 3 | Greyson Jeremia Mushi | Toyota Altezza T527DKY | Dar es alaam | Kasaroba | 28.09.2024 |
| 4 | Ahmed Abdallah Kidondo | Mercedes benz T427 EEL | Dodoma | Marmboto | 28.09.2024 |
| 5 | Regan Aminiel Mahinja | Toyota Noah T524DJA | Arusha | Arm auctioneer | 28.09.2024 |
| 6 | REVOCATUS IBRAHIM SUNDAY | Toyota CALDINA T365AYQ | Dar es alaam | DAR STATE | 28.09.2024 |
| 7 | Mussa Alfani Kilaliyo | Suzuki carry T357DZA | Dar es alaam | DAR STATE | 28.09.2024 |
| 8 | Shaban Daudi Kagomba | Suzuki Carry-T585CYR | Dar es alaam | Kasaroba | 28.09.2024 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355 (Fanikiwa)**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Trump apata kikwazo kingine

**OHIO, Marekani**

FAMILIA moja kutoka Jimbo la Ohio nchini Marekani, amempiga marufuku mgombea wa Chama cha Republican, Donald Trump, kuacha kutumia kifo cha mtoto wake kwa ajili ya kujinufaisha kisiasa.

Mtoto huyo, Aiden Clark (11) alifariki dunia katika ajali ya basi la shule iliyosababishwa na mhamiaji kutika Haiti mwezi uliopita.

Aiden, alifariki katika ajali hiyo iliyotokea katika mji wa Springfield, ambao sasa umekuwa kivutio baada ya Trump kudai wahamiaji kutoka Haiti wanakula wanyama kama mbwa na paka, madai ambayo yalipingwa na uongozi wa jimbo hilo.

Jumanne ya wiki hii, mgombea mwenza wa Trump, JD Vance aliandika ujumbe katika mtandao wa X na kumtaja Aiden kuwa aliuliwa na mhamiaji wa Haiti.

Baba wa mtoto huyo, Nathan Clark, alisema katika mkutano wa ulioandaliwa na tume ya jiji hilo kuwa ujumbe wa mgombea huyo ulirudisha tena majeraha.

„Wamemzungumzia mwanangu na kutumia kifo chake kwa manufaa ya kisiasa. Hili linahitaji kukomeshwa sasa,“ alisema na kuongeza „Mwanangu hakuuawa, alifariki dunia kwa bahati mbaya katika ajali iliyosababishwa na mhamiaji kutoka Haiti.“

Ulisema ujumbe huo umewahuzunisha wengi katika jamii ndani ya majimbo na taifa zima. Alionya kwamba kifo cha mtoto wake isiingize chuki ndani yake.

Saa chache tu baada ya Clark kuzungumzia hilo, Trump alirudia madai hayo jukwaani kwenye mjadala wa urais dhidi ya Makamu wa Rais Kamala Harris.

„Natamani mwanangu, Aiden Clark, angeuliwa na mzungu mwenye umri wa miaka 60, nina hakika hakuna mtu angeweza kusema chochote,“ alisema Clark akiwa na mke wake.

Aiden alifariki wakati lori lililokuwa likiendeshwa na Hermanio Joseph, mhamiaji kutoka Haiti ambaye hakuwa na leseni ya udereva, lilipovuka mstari wa katikati na kugongana na basi la shule.

Mtoto huyo alirushwa nje kutoka kwenye basi hilo wakati lilipopinduka, huku watoto kadhaa wakipata majeraha.

Mahakama ilimkuta Joseph na hatia ya kuua bila kukusudia na kuhukumiwa kifungo cha miaka tisa hadi 13 jela.

***BBC***



Wafungwa wakisafisha sufuria na sahani katika gereza kuu la Makala, nchini DRC katika picha iliyochukuliwa Julai 27, mwaka huu. Jumla ya wafungwa 131 waliuawa wakati wakijaribu kutoroka kwa kupambana na askari hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Zelensky akataa mpango kumaliza vita na Russia

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amekataa mpango wa amani akisema unainufaisha zaidi Russia ambayo imeivamia nchi yake.

Katika mahojiano na mtandao wa Metropoles wa nchini Brazil, alisema mpango huo umependekezwa na serikali za Brazil na China hauna usawa na hauwezi kukubalika.

„Kwa bahati mbaya, nadhani mipango ya Brazil na China inaunga mkono Russia zaidi,“ alisema Zelensky.

Alisema tayari amemtaarifu Rais wa Brazil, Luis Inacio Lula da Silva kuhusu jambo hilo.

Mwishoni mwa mwezi Mei mwaka jana, China na Brazil zilichapisha mapendekezo yao ya kupata suluhu ya vita vinavyoendelea Ukraine.

Katika mapendekezo hayo walisema njia pekee ya kumaliza mzozo huo ni kufanya mazungumzo ya amani na ushiriki ulio sawa wa pande zote.

Wiki hii, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Ryabkov, alisema nchi yake inakaribisha mpango huo.

„Nadhani mpango huu unafurahia kuungwa mkono zaidi na mataifa mengine,“ alisema Ryabkov wakati akizungunza na shirika la habari la RT.

Kulingana na Zelensky, mpango huo wa amani haukukubaliwa na Ukraine, hivyo hawezi kufanya maelewano yoyote na Russia kuhusu maeneo yake.

„Yeye Rais wa Urusi, Vladimir Putin aliingia, akaua watu, akateka eneo na sasa Lula anasema, njoo, waache wazungumze. Ningeweza tu kuzungumza na Lula kwa sababu Lula sio adui yangu,“ alisema Zelensky.

Alisema lazima yeye awe na nguvu ya kukaa chini na kuzungumza juu ya jambo fulani. Lakini anapaswa kuchukua hatua na kuonesha kwamba sio kwa upande mmoja.

***BBC***

## Ndege zaanza kuruka Kenya

**NAIROBI, Kenya**

HUDUMA ya usafiri imerejea katika viwanja vya ndege nchini Kenya, baada ya wafanyakazi kumaliza mgomo kufuatia makubaliano waliyofikiana na serikali.

Katika makubaliano hayo yaliyowarudisha kazini wafanyakazi, serikali itaruhusu kufanyika kwa uchunguzi wa ukodishaji wa miaka 30 wa uwanja wa ndege wa JKIA na kampuni ya Adani ya nchini India.

Gazeti la Nation Daily nchini Kenya, limeripoti kuwa vyama vya wafanyakazi kwenye viwanja vya ndege vya JKIA na Mombasa pamoja na serikali walipata muafaka baada ya mkutano na Waziri wa Uchukuzi, Davis Chirchir.

Viongozi wengine waliohudhuria ni Katibu wa Muungano wa Wafanyakazi nchini humo (COTU), Francis Atwoli.

Waziri Chirchir aliahidi kuwa mkataba ulioafikiwa kati ya serikali na kampuni ya Adani utawasilishwa mahakamani ambapo serikali imeshtakiwa ili kuruhusu uchunguzi wa wazi kufanyika.

Katibu Mkuu wa COTU, Francis Atwoli, alisema kwamba serikali imekubali kuanzisha mazungumzo ya mishahara na wafanyakazi katika kipindi cha miezi miwili.

„Waliamua kuwapatia wafanyakazi hao wa viwanja vya ndege siku 10 kuchunguza stakabadhi hizo za Amani kabla ya mkutano mwengine kufanywa na wadau,“ alisema Atwoli.

***RFI***

## Rais Senegal afikiria kulivunja Bunge

**DAKAR, Senegal**

RAIS wa Senegal, Bassirou Diomaye Faye, anatarajiwa kulivunja Bunge baada ya kukaa madarakani kwa muda wa miezi mitano.

Rais Faye amelazimika kutumia sheria ya kuangalia namna ya kulivunja bunge kutokana na chombo hicho kutawaliwa na wapinzani.

Kiongozi huyo alichaguliwa katika duru ya kwanza ya uchaguzi kwa zaidi ya asilimia 54 ya kura zote, lakini hana wabunge wengi baada ya chama kinachoongozwa na rais wa zamani Macky Sall, kuchukua viti vingi.

Kutokana na serikali yake kutokuwa na nguvu, kuna uwezekano wa kuibuka kwa migogoro endapo hatachukua hatua hiyo haraka.

Chama chake cha PASTEF, kina wabunge 23 pekee kati ya 165 jambo linalompa wakati mgumu wa kupitisha miswada ya kisheria na matumizi ya serikali.

## 200 kushiriki mashindano ya kuogelea

**Na Shufaa Lyimo**

WAOGELEAJI 200 wamethibitisha kushiriki mashindano ya taifa ya wazi ya kuogelea yanayotarajiwa kuanza Septemba 14 kwenye bwawa la kuogelea la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Chama cha Mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), Sebastian Kolowa (pichani), alisema lengo la mashindano hayo ni kuinua vipaji vya vijana.

"Mashindano hayo ni ya wazi, mchezaji yoyote anaruhusiwa kushiriki ili mradi awe amekidhi vigezo vinavyohitajika," alisema Kolowa.

Aidha, alisema mashindano hayo yatashirikisha vijana wenye umri kuanzia miaka saba na kuwataka Watanzania wajitokeze kwa wingi kutazama vipaji.

Aidha, alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vema na kila mchezaji anaendelea kufanya mazoezi yake binafsi.

"Kwa sasa kila mchezaji anafanya mazoezi yake binafsi kuhakikisha anafanya vema katika mashindano hayo ambayo naamini yatakuwa na mvuto wa aina yake," alisema Msemaji Kolowa.



# MAKOCHA TABORA, KAGERA WALIA VIWANGO WACHEZAJI

**Na Adam Fungamwango**

MAKOCHA Francis Kimanzi wa Tabora United na Paul Nkata wa Kagera Sugar, wamesema hawajaridhishwa na viwango vya wachezaji wao katika mchezo uliochezwa juzi, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

Wakizungumza baada ya mechi hiyo ambayo ilimalizika kwa wenyeji Tabora United kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, makocha hao kila mmoja ameonekana kulalamika kivyake kuwa wachezaji wake hawakucheza vizuri.

Kimanzi, alisema wachezaji wake licha ya kuwa na morali ya juu lakini bado wanahitaji kuinua viwango vyao ili waweze kupata matokeo mazuri kwenye michezo inayofuata.

"Wachezaji wangu kuna wakati wanacheza vizuri, wakati mwingine wanacheza vibaya, sikutarajia kama watacheza hivi, tulipata nafasi nyingi lakini hatukuzitumia, sawa wakati mwingine ndiyo mchezo, lakini tunahitaji kuinua kiwango chetu, wanacheza kwa morali, lakini kiwango bado," alisema Kimanzi raia wa Kenya.

Naye Nkata, raia wa Uganda, pamoja na kulalamikia hali ya hewa, alitilia shaka baadhi ya viwango vya wachezaji wake.

"Hali ya hewa iliwaathiri wachezaji wangu kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili tukaizoea, tumecheza vizuri kipindi cha pili kuliko cha kwanza, nadhani kuna baadhi ya wachezaji wangu hawako vizuri kama wachezaji wa timu zingine.

Tutakwenda kukaa chini na kuangalia tatizo ni wachezaji au kocha, lakini ukweli ni kwamba hii ni mechi ya tatu tunapoteza," alisema.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Tabora United kucheza mbele ya mashabiki wake, baada ya michezo miwili kucheza nje, huku ikiwa ni mchezo wa pili kushinda, ikipoteza mmoja kwa mabao 3-0 dhidi ya Simba.

Kwa upande wa Kagera Sugar ni mechi ya tatu mfululizo wanapoteza baada ya kwanza kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Singida Black Stars, ikafungwa mabao 2-0 na Yanga, zote ikicheza nyumbani, kabla ya juzi kukutana na kipigo kingine ugenini.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro (kulia), akikabidhiwa kombe la ubingwa wa michuano ya UNAF na Nahodha wa Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 ,Serengeti Girls', Jamila Rajab, baada ya timu hiyo kurejea nchini kutokea Tunisia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndumbaro aitaka taifa kriketi kufanya vizuri

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, ameitaka Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 19 ya mchezo wa kriketi ihakikishe inakwenda kuipeperusha vema Bendera ya Taifa katika mashindano ya wanawake ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia yatakayoanza Septemba 20 jijini Kigali, Rwanda.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam kwenye hafla ya kuikabidhi Bendera ya Taifa timu hiyo, Ndumbaro alisema serikali wana imani na timu hiyo na kuwataka kwenda kupambana. "Naomba muende mkafanye vizuri katika mashindano hayo ili mpate nafasi ya kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Dunia, tunaamini mnaweza kufanya vizuri," alisema Ndumbaro.

Aidha, alipongeza uongozi wa Chama cha Mchezo huo hapa nchini (TCA) kutokana na juhudi kubwa inayofanya kuhakikisha mchezo huo unachezwa mikoa yote ya Tanzania.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana nao bega kwa bega ili timu hiyo iweze kupata nafasi ya kushiriki michuano hiyo ya dunia.

Kwa upande wake nahodha wa timu hiyo, Agness Joseph alisema kuwa wamefanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha wanakwenda kupata matokeo mazuri katika michuano hiyo.

"Tumefanya maandalizi kwa muda mrefu kuhakikisha tunakwenda kufanya vizuri katika mashindano hayo ili tupate nafasi ya kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Dunia," alisema Joseph.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ANTHONY ASITA KUONDOKA

WINGA wa Brazil, Antony, mwenye umri wa miaka 24, anasita kuondoka Manchester United licha ya Fenerbahce kumtaka. ***(ESPN)***

### TRIPPIER UTURUKI NDIO BASI

KLABU za Super Ligi za Uturuki, Istanbul Basaksehir, Fenerbahce, Besiktas na Eyupspor zimekata tamaa kujaribu kumsajili Kieran Trippier baada ya Newcastle United kuweka wazi kuwa wanataka kusalia na beki huyo wa zamani wa Uingereza mwenye umri wa miaka 33. ***(Sky Sports).***

### ASTON VILLA NA DURAN

KLABU ya Aston Villa imeonesha bado inamthamini na kumwitaji Jhon Duran baada ya hivi karibuni kukataa ofa ya pauni milioni 40 kwa mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

### NEWCASTLE MAMBO SAFI

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe na Mkurugenzi wa Michezo, Paul Mitchell wametatua tofauti zao na sasa wanaangazia uhamisho wa Januari, ikiwa ni pamoja na kumleta beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

### UNITED YAMTAKA SANCHEZ

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa kulia wa Sevilla, Juanlu Sanchez mwenye umri wa miaka 21 ili kumsajili katika dirisha lijalo. (AS)

### CHELSEA UWANJA MPYA

CHELSEA imefanya mazungumzo kuhusu kuondoka Stamford Bridge na kujenga uwanja mpya katika eneo la Earl's Court. ***(Guardian)***

### SPURS ILIMKATAA ROMERO

KLABU ya Tottenham Hotspur ilikataa ofa za kununua beki wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha la uhamisho la majira ya joto. ***(TyC Sports)***

### COOPER KUTUA CSKA SOFIA

MLINZI wa Scotland, Liam Cooper mwenye umri wa miaka 33 anakaribia kujiunga na CSKA Sofia kwa uhamisho huru baada ya kuondoka Leeds United mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Football Insider)***

### EVERTON MBIONI KUNUNULIWA

MFANYABIASHARA wa Marekani, John Textor ana imani kuwa dili la kuinunua Everton linaweza kukamilika baada ya wiki nne. ***(Guardian)***

### MONGAN ATOSWA REAL MADRID

ANDY Mongan wa Stockport County amezuiwa kujiunga na timu ya makocha ya Real Madrid baada ya kunyimwa kibali cha kufanya kazi kwa sababu ya kanuni za Brexit. ***(Times)***

### CHUKWUEMEKA KWA MKOPO

KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20 kutoka England, Carney Chukwuemeka kwa mkopo.***(Teamtalk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ELIOTT MAJANGA WIKI LIVERPOOL

Ni baada ya kuumia kifundo cha mguu na sasa anatarajiwa kukaa nje angalau…

**LIVERPOOL, England**

KIUNGO wa klabu ya Liverpool, Harvey Eliott, anakabiliwa na wiki kadhaa za kuwa nje ya uwanja baada ya kupata majeraha ya kifundo cha mguu akiwa katika majukumu yake ya timu ya taifa.

Nyota huyo anayekipiga katika timu ya vijana wa umri chini ya miaka 21 alipata majeraha hayo wakati timu ya England U21 ilipokuwa ikijiandaa na michezo miwili dhidi ya Ireland Kakazini na Austria.

Kuumia kwa kinda huyo kunampa wakati mgumu kocha wa kikosi cha Liverpool, Arne Slot ambaye bado yupo kwenye tafakari nzito ya utimamu wa viungo, Curtis Jones na Alexis Mac Allister kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu England dhidi ya Nottingham Forest, Jumamosi.

Kwa mujibu wa jarida la The times la nchini England kinda huyo atakuwa nje kwa wiki sita japo Liverpool bado hawajathibitisha.

Eliott anaungana na nyota kama Martin Odegard wa Arsenal na Nathan Ake wa Manchester City ambao pia wanauguza majeraha kutokana na kuumia wakati wakizitumikia timu zao za taifa.

# MBAPPÉ AKATAA USULUHISHI NA PSG

**PARIS,** UFARANSA

KYLIAN Mbappé hayuko tayari kuafikiana na klabu yake ya zamani ya PSG kuhusu madai yake ya fedha.

Nyota huyo wa Ufaransa alikataa ombi la upatanishi la tume ya kisheria ya ligi ya soka ya Ufaransa siku ya Jumatano katika mzozo wake na klabu yake hiyo kuhusu mishahara na bonasi.

Wawakilishi wa Mbappé walikutana na maofisa wa PSG mjini Paris baada ya nyota huyo wa Ufaransa kuitaka tume kuhusika.

Mbappé, ambaye alijiunga na Real Madrid msimu huu kwa uhamisho wa bure, anasema PSG anaidai euro milioni 55.

Katika taarifa kwa ‚The Associated Press‘, wawakilishi wa Mbappé walisema mchezaji huyo aliiomba tume kuzingatia kutolipwa kwa mishahara ya miezi mitatu na theluthi ya mwisho ya bonasi ya uaminifu.

"Hatima ya upatanishi ilitajwa asubuhi ya leo (Jana)," taarifa hiyo ilisema.

"Uwezekano huu ulikataliwa wakati wa mkutano na mwakilishi wa mchezaji. Upatanishi hautakuwa na maana kurekodi ukosefu wa malipo ambao ungeonekana kutokana na uchambuzi rahisi wa bili ya mchezaji."

PSG, walisema walifurahishwa na usikilizaji wa saa mbili katika tume hiyo Jumatano, walisema katika taarifa yao walikumbuka kwamba Mbappé hapo awali alikuwa na „ahadi za wazi, za mara kwa mara za umma na za kibinafsi ambazo lazima ziheshimiwe, baada ya kulipwa faida ambazo hazijawahi kufanywa na klabu zaidi ya miaka saba ya kupendeza huko Paris."

Mabingwa hao wa Ligue 1 wamedai kuwa hawadai fedha kwa mshindi huyo wa Kombe la Dunia chini ya makubaliano



wakati Mbappé alikuwa nje ya uwanja kabla ya msimu wa 2023-24, kufuatia uamuzi wake wa kutorefusha mkataba wake na klabu hiyo huku mchezaji huyo akidaiwa kuwa aliweka bayana kwamba ataachana na bonasi kwa kujumuishwa tena kwenye timu.

PSG ilisema kwamba tume ya kisheria ilipendekeza „Upatanishi kati yao," ambayo klabu ilisema imekuwa ikitafuta kwa miezi kadhaa.

"Kamisheni sasa imemwalika mchezaji huyo kuzingatia mchakato wa upatanishi," alisema msemaji wa PSG.

Uhusiano wa Mbappé na PSG ulimalizika huku kukiwa na mvutano mkubwa wakati wa msimu wake wa mwisho katika klabu hiyo.

PSG ilihisi kukatishwa tamaa na Mbappé baada ya kumpa mkataba mnono zaidi katika historia ya klabu hiyo aliposaini mkataba mpya mwaka wa 2022. Lakini Mbappé alichanganyikiwa kwa sababu alihisi ahadi za kusajili wachezaji muhimu hazikutimizwa.

Aliposaini mkataba huo mpya, alifanyiwa gwaride mbele ya mashabiki akiwa ameshikilia jezi yenye namba 2025 ndani yake. Mbappé aliripotiwa kukasirishwa na hili kwa sababu mkataba ulikuwa hadi 2024 na chaguo la kuongeza mwaka mmoja zaida.

Mbappé aliishangaza PSG Juni mwaka jana kwa kuitaarifu klabu hiyo kwamba hatachukua chaguo hilo kwa mwaka mmoja zaidi. Huku mkataba wake ukiwa umekamilika mwaka wake wa mwisho, PSG waliwekwa katika nafasi ya kuhitaji kumhamisha Mbappé ili kuepuka kumpoteza bure mkataba utakapomalizika.

Uchezaji wake wa PSG ungeisha msimu wa joto wa 2023 huku kukiwa na mvutano mkali wa uhamisho.

Baada ya kuiambia klabu kuwa hataongeza mkataba wake kwa mwaka mmoja zaidi, Mbappé aliachwa katika ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Japan na Korea Kusini na kulazimika kufanya mazoezi na wachezaji wengine.

PSG walisema afadhali kumuuza kuliko kumwacha mchezaji huyo aondoke bure mwaka 2024, lakini alikataa uhamisho wa euro milioni 300 kwenda timu ya Saudia ya Al-Hilal.

PSG ilimwacha Mbappé kwenye mchezo wa ufunguzi wa ligi ya timu hiyo msimu huo huku mvutano ukiendelea, lakini hatimaye wakamruhusu kurejea kwenye kikosi baada ya „mazungumzo chanya ya kujenga" kati ya pande hizo mbili, PSG ilisema wakati huo.

## Ødegaard aipa matumaini Arsenal

**LONDON,** ENGLAND

NAHODHA wa Arsenal, Martin Ødegaard anaweza kukabiliwa na wiki kadhaa nje ya uwanja baada ya kuumia kifundo cha mguu wa kulia wakati akiisaidia nchi yake ya Norway kushinda 2-1 dhidi ya Austria kwenye Ligi ya mataifa ya Ulaya.

Ødegaard alipanda ndege kurejea London akiwa na maumivu ambako alifanyiwa uchunguzi zaidi kubaini ukubwa wa jeraha hilo.

Arsenal watamenyana na wapinzani wao wa London Kaskazini, Tottenham Hotspur katika Ligi Kuu ya England Jumapili wakati pia watakuwa bila kiungo Declan Rice ambaye amesimamishwa.

„Majeraha kama hayo ya kifundo cha mguu mara nyingi huchukua angalau wiki tatu, lakini inaweza kuchukua muda mrefu," alisema daktari Ola Sand akiiambia VG ya Norway.

"Majeraha ya kifundo cha mguu yanaumiza sana, kwa Martin, alikuwa na uchungu sana, alipata wasiwasi sana.

"Tulichopata hadi sasa kutokana na uchunguzi wa MRI huko London ni kwamba pengine hakuna mvunjiko kwenye kifundo cha mguu. Katika tukio la kuvunjika, tunazungumza juu ya kuwa nje ya uwanja kwa wiki sita zaidi."

Ødegaard amekuwa mtu wa kuvutia sana Arsenal na amekosa mechi chache tu za Ligi katika misimu mitatu iliyopita chini ya kocha mkuu Mikel Arteta.

Kukosekana kwa muda mrefu kungekuwa pigo kubwa kwa Arteta hasa kutokana na mchezaji mpya, Mikel Merino naye kuwa nje baada ya kuvunjika bega.

Baada ya mechi dhidi ya Tottenham, Arsenal wataanza kampeni yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta Alhamisi ijayo.



## Ronaldo: Man Utd inahitaji kujengwa upya

**LONDON,** ENGLAND

CRISTIANO Ronaldo ameonya kwamba Manchester United inahitaji kujengwa upya baada ya Sir Jim Ratcliffe kuwekeza katika klabu hiyo, na akashughulikia kuondoka kwake kwa kishindo.

Huku Ratcliffe akiwa amepata asilimia 27.7 ya hisa za United mapema mwaka huu, Ronaldo ana matumaini kuhusu mustakabali wa timu hiyo lakini ameonya kwamba kurejea kwenye daraja la juu la soka la klabu kutahitaji uvumilivu.

"Wanahitaji kujijenga upya kwa kila kitu, kwa maoni yangu," alisema Ronaldo mwenye umri wa miaka 39.

"Klabu hii inahitaji muda wa kujijenga upya kwa sababu bado ni moja ya klabu bora zaidi duniani, lakini wanahitaji kubadilika. Wanaelewa hilo. Hii ndiyo njia pekee, wanawekeza kwenye uwanja wa mazoezi. Kwa hivyo mimi ‚Nina furaha kwa sababu mambo yanabadilika, ninaamini kuwa siku zijazo zitakuwa nzuri.

"Lazima wajenge upya kutoka chini. La sivyo, hawawezi kushindana. Haitawezekana. Wanaweza kufanya mambo mazuri, ndio, wanaweza kushinda Carabao, lakini ninamaanisha, Ligi ya Mabingwa Ulaya au Ligi ya Europa au Ligi Kuu ni ngumu, kwa maoni yangu."

Ronaldo alihamia Saudi Arabia baada ya kuondoka na amekuwa na jukumu kubwa akiwa na Al Nassr, ingawa bado hajabeba taji lolote katika taifa hilo la Ghuba.

"Sina furaha jinsi yote yalivyotokea, lakini kwa njia hiyo hiyo, hatuwezi kudhibiti baadhi ya pointi za maisha yetu wakati mwingine," alisema Ronaldo.

"Ili kuthibitisha kuwa mimi ni sawa au si sahihi, hili sio suala langu tena."

Ronaldo aliachana na klabu ya Manchester kwa maelewano kufuatia mahojiano makali na Piers Morgan ambapo aliikosoa klabu hiyo kwa kushindwa kuwekeza katika kipindi cha miaka 13 tangu alipoondoka Old Trafford kwa mara ya kwanza.

Alisema hajutii kujiunga tena na United kutoka Juventus mwaka 2021 ingawa uhamisho huo haukufanikiwa, na akasema anatumaini „zuri" licha ya kuondoka kwake kwa bahati mbaya Novemba 2022.

"Nilisema ninachotaka kusema na kwangu imekamilika," alisema Ronaldo. „Lakini kuwa mkweli kwako, ninachotamani kwa Manchester United, ndicho ninachotamani kwangu. Bora zaidi wanaweza kutengeneza tena timu bora wanayoweza kuwa nayo na ninaipenda klabu hiyo, unajua mimi sio mtu wa aina ya kusahau nilipotoka au nilipopita".

"Niliporudi huko, nilifurahi sana," Ronaldo aliongeza. „Nilikuwa mmoja wa wafungaji bora. Nilifanya mambo ya ajabu na klabu na bado nayakumbuka," alisema Ronaldo.

Ronaldo, ambaye alifunga jumla ya mabao 145 katika mechi 346 alizochezea United katika misimu yake miwili, alikiri kuwa alikuwa na matatizo na mawazo ya Kocha Erik ten Hag.

"Kocha wa Manchester United, huwezi kusema kwamba hutapigana kushinda Ligi au Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Ronaldo.

HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION YAMKANA MGUNDA

Na Adam Fungamwangwo

KLABU ya Coastal Union imekana kutaka kumrudisha kocha wake wa zamani, Juma Mgunda ili kukinoa kikosi hicho.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema taarifa za Mgunda kutaka kurejea Coastal Union si za kweli, lakini akakiri kuwa viongozi wapo kwenye mchakato wa kusaka Kocha Mkuu na watu wa benchi la ufundi.

Sabri, alisema Coastal imelazimika kutoa ufafanuzi huo kutokana na taarifa nyingi ambazo zinaihusisha timu hiyo na Mgunda, ambaye amemaliza mkataba wake wa miaka miwili na klabu ya Simba.

„Hakuna taarifa yoyote juu ya Juma Mgunda kwenye klabu yetu, tunajua yeye alikuwa mchezaji wetu zamani na alihudumu kwa mafanikio makubwa, pia alikuwa kocha na kufanya mambo makubwa, kusema hatumuhitaji ni kumkosea heshima, lakini kwa sasa hakuna mipango hiyo ya kuzungumza naye, badala yake uongozi bado unaendelea na mchakato wa kumsaka Kocha Mkuu na watu wa benchi la ufundi, lakini siyo Mgunda, timu iko chini ya Kocha Joseph Lazaro ambaye anakaimu na amekuwa akifanya vizuri na viongozi wameonyesha kuwa na imani naye,“ alisema El Sabri.

Tetesi zinasema kuwa klabu zilizokuwa zikimtolea macho Mgunda ni Coastal na Namungo.

Kabla ya kutua Simba, Mgunda alikuwa kocha wa Coastal na alichukuliwa kuziba nafasi ya Zoran Maki ambaye aliondoka mapema kwenye klabu hiyo kabla ligi wala michezo ya kimataifa haijaanza, aliwezesha kutinga hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), akicheza ngoma wakati wa Maonesho ya 25 ya Kimataifa Buildexpo Afrika 2024 yanayofanyika katika ukumbi wa Daimond Jubilee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sare yaikera KVZ FC Zanzibar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

Matokeo ya sare waliyoipata juzi KVZ FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar yameikera klabu na kuapa kupambana kwenye michezo ijayo ili kupata pointi tatu.

Kocha wa timu hiyo, Ali Mohamed, alisema matokeo hayo waliyoyapata dhidi ya Tekeleza FC hayakuwa mipango yao kwa kuwa walijiandaa na kujipanga kupata ushindi.

“Pamoja na yote washambuliaji wangu walishindwa kutumia nafasi ambazo tulizitengeneza, haya hayakuwa matokeo tuliyoyategemea,“ alisema Mohamed.

Aidha, alisema wanakwenda kufanyia kazi mapungufu waliyoyaona ili kupata matokeo mazuri kwenye michezo inayofuata.

Alisema safu hiyo ya ushambuliaji kiufundi ilicheza namba pungufu katika eneo la mbele wakati wanamiliki mpira hali iliyopelekea kupoteza mipira mingi.

Alisema kwa ujumla kikosi chake kilicheza vizuri lakini suala la umakini na kushindwa kufanya maamuzi ya haraka wakati wanashambulia ndio iliyosababisha kutopata ushindi.

“Tulicheza vizuri, tulitengeneza nafasi nyingi sana lakini washambuliaji wangu walishindwa kuzitumia kutokana na sababu nilizoeleza,“ alisema Mohamed.

Hata hivyo alisema wanarejea nyumbani ‚Unguja‘ kujipanga na mchezo wao watatu ambao watashuka uwanjani Septemba 15 kucheza dhidi ya Chipukizi FC.

## Wachezaji Simba waahidi ushindi

INATOKA UK. 24

Kikosi cha Simba kilitua jana hiyo hiyo nchini Libya baada ya kuondoka Uturuki.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuondoka Istanbul, Meneja wa kikosi hicho, Patrick Rweyemamu, alisema waliondoka na kikosi cha wachezaji 17, viongozi na benchi la ufundi, huku baadhi ya wachezaji wakitarajia kuwakuta nchini humo.

“Tupo makundi mawili, wengine wanatoka kwenye vikosi vya timu za taifa, wao waliunganisha moja kwa moja Libya, sisi hapa tuna wachezaji 17, benchi la ufundi na viongozi,“ alisema.

Baada ya mechi hiyo, mchezo wa marudiano unatarajiwa kuchezwa, Septemba 20, Uwanja wa Banjamin

## Yanga ‘yamshupalia’ Kagoma

INATOKA UK. 24

ilimtumia tiketi ya ndege kutoka Kigoma hadi Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya maongezi na Machi 28 alisaini mkataba wa miaka mitatu mbele ya mwanasheria wake na ulitakiwa kuanza kufanya kazi Julai Mosi mwaka huu,“ alisema.

Hata hivyo alidai baadaye ilipokea barua kutoka Singida Fountain Gate ikisema malipo yale yabadilishwe yawe ya mchezaji Nickson Kibabage ambaye yupo Yanga kwa mkopo.

“Julai 6 tuliwaingizia Shilingi milioni 30 kwa ajili ya mchezaji Kibabage, pesa ya Kagoma ikabaki pale pale.

Kwa maana hiyo Kagoma ana mkataba na klabu mbili na sababu ya kupeleka Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ilikuwa ni kuvunja mmoja ili mchezaji awe wa timu moja, suala hili halijasikilizwa.

Hivi karibuni klabu ya Fountain Gate ilisema ilishamalizana na Simba, ambapo wanavyojua Kagoma ni mchezaji halali wa klabu hiyo baada ya kutimiza matakwa yote ya mkataba.



Michezo

Ijumaa Septemba 13, 2024

Nipashe

**Eliott majanga Liverpool**

UKURASA 21



# Wachezaji Simba waahidi ushindi

## ●●●Wakongwe wa timu hiyo wamesema mashindano ya kimataifa ndio wanayo...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kikiwasili jana jijini Tripoli Libya kwa ajili ya mchezo wa raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli Jumapili kwenye Uwanja wa Juni 11, wachezaji wa timu hiyo wamesema wanaanza kucheza michuano ya kimataifa ambayo wanaipenda na kuahidi ushindi kwenye mchezo huo.

Wakizungumza wakiwa Uwanja wa Ndege jijini Istanbul nchini Uturuki jana kabla ya kuunganisha ndege kuelekea Libya, wachezaji wa timu hiyo wamesema kama kuna wakati huwa wanafurahi, basi ni kushiriki michuano ya kimataifa iwe ya Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho.

Beki mkongwe wa timu hiyo, Shomari Kapombe, amesema kwa vyovyote vile hawawezi kukubali kupoteza mechi hiyo kwani wanataka kuendelea kucheza michuano walioizoea ambayo wanaipenda, michuano ya kimataifa.

"Hiki ndicho kipindi ambacho wanachama na mashabiki wa Simba wanakipenda kuliko kipindi chochote kile, hiki ni kipindi cha michuano ya kimataifa na hata sisi wachezaji ndiyo wakati ambao tunaupenda sana, kikubwa cha kuwaambia mashabiki wetu kuwa matarajio yetu ni makubwa sana kuna wachezaji wengi wapya wenye ari, nguvu na kujituma na wenye kujitolea, hiki kitu kimekuja kuongeza morali katika kikosi chetu, sasa umefika wakati wa kwenda kufanya kwa vitendo kwa sababu muda wa maandalizi umeisha, niseme tu kuwa kila mchezaji yupo tayari kwa huu mchezo," akisema Kapombe.

Kiungo mshambuliaji mpya wa timu hiyo aliyesajiliwa kutoka KMC, Awesu Awesu, amesema wanachama na mashabiki wa Simba wanapenda sana kuona timu yao ipo kwenye hatua ya makundi Afrika na huwa hawajisikii vizuri kama haipo kwenye hatua hiyo.

"Mimi tangu nipo KMC, nawaona kabisa kuwa mashabiki wa Simba hata kama wasipofanya vyema kwenye ligi, lakini kama wako kwenye hatua za makundi michuano ya kimataifa wanafurahi sana, yaani tunatakiwa kufanya tufanyavyo ili wajisikie wenye furaha, wanaihitaji hatua hii," alisema Awesu.

INAENDELEA UK. 23



Kapombe

# Yanga SC 'yamshupalia' Kagoma

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga bado imeendelea kumng'ang'ania mchezaji Yusuph Kagoma, ikisema ni mchezaji wao halali na alisaini mkataba wa miaka mitatu, Machi 28, mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Sheria wa Klabu ya Yanga, Mwanasheria, Simon Patrick, amesema tayari suala hilo wamelipeleka kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ila bado halijafanyiwa kazi ili kutoa uamuzi.

Amesema lengo la kuliweka hadharani jambo hili ni kutaka wanachama, mashabiki wa wadau wengine wa soka walielewe kwani limekuwa na sintofahamu kubwa.

Kagoma kwa sasa ni mchezaji wa Simba aliyesajiliwa kutoka Fountain Gate na yupo nchini Libya kukitumikia kikosi hicho ambacho Jumapili kitacheza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli.

Mwanasheria ambaye alionyesha karatasi za malipo ya pesa kwa klabu ya Singida Fountain Gate na mkataba wa mchezaji huyo, aliitaka kamati hiyo kuamua mambo matatu, kutamka kuwa Kagoma ni mchezaji wa Yanga, pili isimamie kanuni zake kwamba mchezaji anayesaini zaidi ya klabu moja afungiwe, au watoe adhabu na fidia ya kuvunjwa mkataba wao kihuni.

"Machi 4, mwaka huu klabu ya Yanga kupitia kamati ya utendaji walianzisha mchakato wa kumnunua kutoka Singida Fountain Gate, baada ya muda mwafaka kufika Fountain Gate ilitoa masharti kuwa ni lazima ilipwe Shilingi milioni 30.

Kipengele kinasema Yanga italipa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza shilingi milioni 15 na mwisho ilikuwa mwezi Aprili na awamu ya pili ni mwezi Juni," alisema.

Alisema, Yanga walifanya hivyo na rasmi mchezaji huyo kuwa mali ya Yanga, na iliruhusiwa kufanya mazungumzo na mchezaji.

"Tarehe 27, Machi mwaka huu

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042